Nipashe
Jumamosi Aprili 6, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581638
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Uingereza** kuipatia Tanzania trilioni 3/-
UKURASA 3

**Wagonjwa** wapya 40,000 wa saratani hubainika kila mwaka
UKURASA 4

**Hatima** hukumu kesi rufani ya Gekul Aprili 15
UKURASA 15



PARTEY : SINA MPANGO WA KUONDOKA ARSENAL
UKURASA 22



# Mbunge ataka tozo za simu kunusuru NHIF



• **Ummy** asema suluhisho mvutano na sekta binafsi laja... *Endelea Ukurasa 2 & 5*

UKURASA WA 5

## MAKALLA: NAYAJUA MAJUKUMU YANGU

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amesema nafasi aliyopewa anafahamu majukumu yake na yeye na wenzake...

## Serikali yashauriwa kupunguza utegemezi wa afua za UKIMWI

UKURASA 2



Wataalamu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na wenzao kutoka India, wakimfanyia upasuaji mgonjwa kwa njia ya tundu dogo kwa kutumia kifaa maalumu (Stent) kurekebisha mshipa wa damu uliotanuka sehemu ya kifua, katika taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Wagonjwa watano watafanyiwa upasuaji huo ambao kwa mara ya kwanza umefanyika nchini kwa kutumia mtambo wa Cathlab. **Habari Uk.7. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wenyeviti wadaiwa kuuza eneo la maziko

UK. 3

**MICHEZO** **MAYELE : NINAWEZA KUJIUNGA SIMBA SC** UK.24

**MAONI,** UK.6

## Serikali yashauriwa kupunguza utegemezi afua za UKIMWI

**Na Vitus Audax,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, imeshauri serikali kupunguza utegemezi wa kiwango kikubwa katika fedha za udhamini kutoka nje kufadhili afua mbalimbali za kuratibu masuala ya UKIMWI.

Imesema kwa kufanya hivyo, inatishia usalama wa watu waishio na virusi vya UKIMWI (WAVIU) pale wafadhili watakapositisha kutoa fedha hizo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, aliyasema hayo juzi bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha maoni ya kamati hiyo, kuhusu utekelezaji wa Kazi za Serikali na Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania-TACAIDS) kwa mwaka wa fedha 2023/24 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

Nyongo alisema kwa fedha za maendeleo za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) ni Sh. bilioni 1.88 ambazo zitatumika katika maeneo makuu matatu na asilimia 60 ni kuwezesha upatikanaji wa huduma za kuzuia VVU na utoaji elimu ya VVU na UKIMWI.

Alisema asilimia 30 zimeelekezwa kuwezesha uendeshaji wa mfuko ikiwamo kugharamia vikao vya kisheria vya kila robo mwaka vya bodi ya mfuko na utafutaji wa rasilimali za kuutunisha.

Pia alisema asilimia 10 ni kwa ajili ya kukabiliana na madhara ya UKIMWI ikihusisha kuwawezesha WAVIU kiuchumi.

"Licha ya kupungua kwa fedha za bajeti ya maendeleo kutoka nje, bado bajeti kwa kiasi kikubwa inategemea fedha kutoka nje. Hali hiyo bado ni tatizo kutegemea fedha za wafadhili kwa kiwango kikubwa katika kuratibu masuala ya UKIMWI jambo ambalo linatishia usalama wa WAVIU pale wafadhili watakapositisha kutoa fedha hizo," alisema Nyongo.

Alisema kamati inashauri serikali itoe fedha zote za TACAIDS kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa muda uliopangwa.

Pia alisema kamati inashauri serikali iimarishe Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI na kuweka mipango madhubuti ya kupata vyanzo mahsusi vya mapato ya ndani vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya miradi inayolenga kudhibiti VVU na UKIMWI.

Nyongo alisema serikali iongeze kiwango cha fedha za ndani inazotenga kupitia ATF kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa afua mbalimbali za kudhibiti UKIMWI bila kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi.

**GEREZANI**

Kuhusu utekelezaji wa afua za UKIMWI gerezani, Nyongo alisema serikali imekuwa ikizitekeleza ili kudhibiti maambukizi ya UKIMWI katika magereza yote nchini.

Alibainisha afua hizo ni pamoja na kuboresha na kuimarisha mapambano dhidi ya UKIMWI gerezani.

Nyongo alisema kamati inaishauri serikali isimamie utekelezaji wa mwongozo wa utoaji huduma kwa wafungwa na mahabusu uliotolewa Mei 25, 1998, na Wizara ya Afya, ambao ulielekeza jukumu la kuwatibu wafungwa na mahabusu ni la Mganga wa Hospitali ya Serikali katika eneo gereza husika.

Pia alisema alisema serikali ihakikishe kuna upatikanaji wa uhakika wa dawa magerezani kwa ajili ya kutibu wafungwa na mahabusu hususani wakati wa dharura.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Deogratius Ndejembi (kushoto), akipongezwa na aliyekuwa waziri wa wizara hiyo, Prof. Joyce Ndalichako walipokutana Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge ataka tozo mitandao simu, mazao kunusuru NHIF

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MBUNGE wa Gairo, Ahmed Shabiby, ameiomba serikali kuweka tozo ya Sh.2, 000 kwa mwezi katika mitandao ya simu pamoja na mazao ili kuusaidia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuendelea kujiendesha na kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Akichangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2024/25, Shabiby alisema hatua hiyo itakuwa mkombozi kwa mfuko huo ili kuondoa malalamiko ya mara kwa mara.

"Kwa hili wanaweza kulikubali au wasilikubali wengine watatukana kwenye mitandao, lakini acha watukane maana kuna watu hawapo duniani na hata mbinguni hawako. Wako katikati wanaelea, lakini siwezi kuogopa kwa sababu mtu atatukana.

"Ili kuinusuru bima ya afya, kuna umuhimu wa kuwapo chanzo ambacho kitakuwa cha uhakika katika kuchangia mfuko huo kwani wananchi wameshindwa kuchangia Sh. 30,000 kwa ajili ya bima ya CHF na hivi hatujajua hiyo bima kwa wote itakuwa na kiwango kipi," alisema.

Shabiby alisema ikipangwa Sh.300,000 na Sh.60,000 kwa matibabu ya kawaida wananchi wa maeneo ya vijijini kuimudu itakuwa vigumu, hivyo kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi kama inavyohitajika, hivyo ni wakati wa wananchi kujionea huruma ili kuokoa mfuko huo.

"Ukiangalia katika mipango ni kutaka kuwachangisha wananchi lakini namna ya kupata hii fedha itakuwa vigumu kama ilivyokuwa kwa CHF na leo hii ukiangalia wanufaika wa bima katika watanzania 100 ni watu wanane tu ambao wanalipa bima.

"Hii inaonyesha hatuna chanzo maalum cha kuchangia mfuko huu, kwakusaidia watu wasiyokuwa na uwezo wapate matibabu,"alisema.

Alitaja njia za kupata chanzo hicho cha uhakika kuwa ni pamoja na kuweka tozo katika mitandao ya simu ambayo inatumiwa sana nchini, zikiwapo zaidi ya laini milioni 72. Alisema ikiwekwa tozo ya Sh. 2,000 kwa mwezi kwa mwaka itakuwa Sh. 24,000 sawa na Sh. trilioni 1.728 kwa idadi ya laini hizo.

Mbunge huyo alishauri pia watumiaji wa mitandao hiyo wenye hadhi kama vile wabunge, wafanyabiashara, wafanyakazi kiwango kiongezwe hadi Sh.10,000 au 15,000 na kuunganishwa na kupatikana zaidi ya Sh.trilioni mbili.

"Pamoja na kuwapo kwa kiwango hicho, wananchi wa vijijini wasiwekewe ukomo wa matibabu kutokana na kuwa na kipato kidogo ambapo wamekuwa wakikosa matibabu na dawa za muhimu," alisema.

Shabiby alisema viwango vingine vitafutwe hata kwenye mazao ambako kila kilogramu moja itatozwa Sh. moja au mbili kwa kuwa hata mkulima atanufaika na bima hiyo.

"Sasa kwa wale ambao hawana simu, hiyo inadhihilisha kuwa ni maskini wa kutupwa, hivyo hata hicho kiasi kidogo wasitozwe, atatibiwa kutokana na vyanzo hivyo vya mifuko," alisisitiza.

**VITUO VYA AFYA, ZAHANATI**

Mbunge Shabiby alishauri zahanati za vijiji pamoja vituo vya afya vibinafsishwe akitolea mfano, nchi ya Korea Kusini ambako wamefanya hivyo kwa kuwekwa kwenye mfumo mmoja, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utolewaji wa huduma za afya.

Alisema kuwapo kwa mfumo huo wa ufuatiliaji wa vituo vyote vya kutoa huduma za afya, utasaidia kudhibiti vitendo vya udanganyifu katika mfuko wa bima ikiwa ni pamoja na kusaidia ongezeko la wahudumu wa afya.

**UTITIRI TOZO UVUVI**

Mbunge wa Ilemela (CCM), Angelina Mabula, katika mchango wake aliomba serikali katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25, itazame namna ya kuondoa utitiri wa tozo kwa wavuvi ili kudhibiti utoroshaji wa mazao ya samaki kwenda nje.

Mabula alisema ongezeko la ushuru wa mazao ya samaki kutoka Sh. 10 hadi Sh. 100 kwa kila kilo moja kunawaumiza wafanyabiashara na wavuvi, hali inayosababisha ongezeko la watu wanaouza na kusafirisha kwa magendo mazao hayo kwenda nje kinyume cha sheria.

Pia aliomba serikali kuongeza umakini katika kudhibiti wa utapeli mitandaoni kwa kuwa umezidi kushamiri hadi kwa viongozi, akijitolea mfano. Alisema licha ya mamlaka husika kusajili laini zote kwa alama za vidole, kuna watu walikuwa wakijitambulisha kwa jina lake na kutapeli watu.

HABARI KITAIFA

# Viongozi wadaiwa kuuza eneo la maziko

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WENYEVITI wa Serikali za Mitaa ya Bukondamoyo na Shunu katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, wanadaiwa kuuza eneo la maziko lenye ukubwa wa ekari 23.

Kitendo hicho kimedaiwa kimesababisha kuwapo kwa ujenzi holela maeneo hayo kinyume cha sheria, hivyo kuchangia wananchi kukosa eneo la maziko.

Kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, wenyeviti hawaruhusiwi kusimamia mauziano ya ardhi na badala yake, wanatakiwa kumtambulisha mnunuzi kwa mmiliki halali wa eneo husika na si kusimamia na utiaji saini wa nyaraka.

Sheria hiyo imeweka wazi kuwa kama eneo litakuwa la umma au wazi, wanatakiwa kushauri na kusitisha biashara.

Wakizungumza mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, katika mkutano alioitishwa kusikiliza na kutatua kero za wananchi, wakazi hao walisema wenyeviti wa serikali za mitaa wamekuwa chanzo cha migogoro ya ardhi kwa kuuza maeneo ya wazi na umma kinyemela.

Mkazi wa Mtaa wa Shunu, Ezekieli Malale, alisema eneo lenye ekari 23 lililotengwa na halmashauri kwa ajili ya maziko limevamiwa na wananchi na kuanzisha makazi ya kudumu.

Malale alisema hali ambayo inayofanya wakati wowote eneo hilo kujaa na walipofuatilia uuzaji huo, walibaini wenyeviti wa mitaa ndiyo wanaohusika.

"Eneo hili liko mpakani mwa Kata ya Nyahanga na Mhungula, Mwenyekiti wa Mtaa wa Shunu na Bukondamoyo, wanadaiwa kuliuza kwa wananchi na kujengwa makazi ya kudumu.

"Tunaomba serikali ingilie kati na kuwaondoa waliouziwa kinyemela ili tupate mahala pakuzika watu watakapofariki," aliomba.

Michael Mussa, alisema yeye aliuziwa kiwanja kwa Sh. 550,000 kando ya Bwawa la Mtakuja na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Shunu, Japhet Kaliwa, na wakati anaanza ujenzi wa makazi, alizuiwa kuwa ni eneo la umma.

Mwananchi huyo alimwomba mkuu wa wilaya kumsaidia ili kurejeshewa gharama alizotumia au kufidiwa eneo lingine.

Mkazi mwingine, Aidani Daniel, alisema wengi wao wamejenga makazi ya kudumu kiholela na viwanja vyao havikupimwa na kushauri Idara ya Ardhi kuyapima maeneo yao na kupanga mji ili wasiendelee kujenga kiholela.

Alisema kulingana na wananchi walivyojenga, likitokea janga la moto, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halitapata sehemu ya kupita.

Akijibu malalamiko hayo, Mahugi alidai hakushiriki kuuza eneo la maziko lililotengwa na serikali bali aliyefanya hivyo ni Kaliwa na yeye ndiye aliyetoa taarifa hiyo ofisi za Kata, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na halmashauri.

Alisema kutokana na kutochukuliwa suala hilo kwa ukubwa, kulisababisha zaidi ya nyumba 80 kujengwa, hatua iliyowafanya kurasimisha kwa waliojenga na eneo lililobaki ndilo litatumika kama sehemu ya maziko.

Aidha, alisema waliojenga maeneo hayo wamekuwa mabalozi wazuri ili eneo hilo lisiendelee kuvamiwa.

Mhita aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuvamia maeneo ya wazi na kuanzisha ujenzi wa makazi, kwani kufanya hivyo kunachangia kuwapo kwa migogoro ya ardhi.

Pia alimtaka mwenyekiti wa serikali ya mtaa aliyechukua Sh.550,000 baada ya kuuza eneo la Bwawa la Mtakuja la serikali, kumrejeshea mwananchi huyo.

# Uingereza kuimwagia Tanzania tril. 3/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA na Uingereza zimetia saini mkataba wa makubaliano wa ushirikiano wa miaka mitano wenye thamani ya Sh. trilioni tatu unaolenga kukuza maendeleo katika sekta za afya, uwekezaji wa kijamii na ukuaji wa uchumi jumuishi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema katika mkataba huo, eneo la kuchochea biashara na uwekezaji zitatolewa Sh. bilioni 300.

"Leo nimekutana na Waziri wa Uingereza wa Maendeleo na Afrika, Andrew Mitchell, tumeshuhudia utiaji saini wa mkataba wa ushirikiano kwa ajili ya ustawi kati ya Tanzania na Uingereza.

"Mkataba huu umetiwa saini kati ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ,Dk. Tausi Kida na Balozi wa Uingereza Nchini, David Concar, na katika maeneo haya ya biashara na uwekezaji tunatarajia zipatikane Paundi za Uingereza milioni 100 sawa na Sh.bilioni 300,"alisema.

Kadhalika, alisema katika mkataba huo Tanzania itashirikiana na Uingereza kufanya uwekezaji katika madini ya kimkakati, utajikita katika kuongeza thamani nchini.

"Lengo la Rais Samia Suluhu Hassan ambalo amelisukuma sana ni kuongeza thamani mazao yetu ya madini husuan madini ya kimkakati ambayo yanahitajika sana katika Green Environment katika kutengeneza betri, kwa hiyo jambo hili tumelipokea vizuri kwa kuwa, linalenga kwenda kutuongezea uwezo wetu sisi wenyewe,"alisema.


Nipashe The Guardian

Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited



**Wapendwa Wateja wetu**

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia wikiendi ijayo ya tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya Nipashe na The Guardian yatakuwa yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

# Wagonjwa wapya 40,000 wa saratani wabainika kila mwaka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAGONJWA wapya 40,000 wa saratani hubainika kila mwaka nchini huku wanaofika hospitalini kupata matibabu ni kati ya asilimia 28 na 30, Bunge lilielezwa jana jijini hapa.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alibainisha hayo jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo. Mbunge huyo alitaka kujua kama serikali haioni umuhimu wa kupeleka huduma ya mionzi katika Hospitali ya rufani ya Kanda ya Kusini iliyoko Mtwara.

Alisema wagonjwa wengi wa saratani wanakwenda hospitalini wakati hali imekuwa mbaya.

"Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inatoa elimu ya kutosha kwa wanawake wengi ambao wako vijijini ili watibiwe magonjwa haya kwa wakati?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Ummy alisema Tanzania inakadiriwa kila mwaka kugunduklika wagonjwa wapya 40,000 wa saratani, lakini wanaofika kupata huduma ni asilimia 28 hadi 30.

Ummy alisema kati ya hao wanaofika kupata huduma, asilimia 70 hufika wakati saratani ikiwa katika hatua ya tatu au ya nne ambayo ni ngumu kutibu au matibabu kutumia muda mrefu.

"Tunahitaji elimu kwa wananchi ya kupima saratani kwenye mikutano kuwakumbusha kupima saratani kwa kuwa inatibika ikigundulika mapema," alisema.

Ummy alisema serikali ina mpango wa kujenga huduma za saratani kwa njia ya mionzi Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini Mtwara kwa mwaka 2025/26 na kwa sasa wanakamilisha katika Hospitali ya Kanda Nyanda za Juu Kusini ambayo inajumuisha mikoa mingi na ile ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC mkoani Kilimanjaro.

Katika swali la msingi, Mbunge Malapo alitaka kujua ni hospitali ngapi zinatoa huduma ya tiba ya mionzi kwa wagonjwa wa saratani.

Waziri Ummy alisema kwa sasa serikali ina vituo vinne ambavyo vinatoa huduma ya matibabu ya saratani nchini kwa njia ya mionzi. Alivitaja vituo hivyo kuwa ni Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Hospitali ya Kanda ya Bugando, hospitali ya binafsi Besta na Hospitali ya Good Sammaritan (St. Fransis Ifakara).

Alisema serikali inaendelea na taratibu za uwekezaji kwa kuongeza vituo vingine vitatu (Hospitali ya Benjamin Mkapa, KCMC na Hospitali ya Kanda Mbeya) kwa Tanzania Bara na kimoja kwa Visiwani Zanzibar (Hospitali ya Binguni) kwa kujenga majengo na kuviwezesha vifaa vitakavyotumika kutibu wagonjwa wa saratani kwa njia ya mionzi.




Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam jana kwenye mkutano wa kutangaza maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari yatakayofanyika Dodoma Mei 3 mwaka huu. Kushoto ni Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa (UNESCO), Michel Toto na Rais wa Umoja wa Vilabu vya Waandishi wa Habari (UTPC), Deogratius Nsokolo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tembo waliovamia makazi waanza kurejeshwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeanza kurejesha makundi ya tembo katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ambayo yamevamia makazi ya watu katika vijiji vya Mangae, Doma na Mkata, mkoani hapa.

Mchakato wa kuwarejesha unaendelea mpaka sasa, tayari makundi matatu yenye tembo 45 yamerejeshwa hifadhini.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dunstan Kitandula, aliyasema hayo katika kijiji cha Mangae, wilayani Mvomero, wakati wa uzinduzi wa operesheni hiyo ya kurudisha makundi hayo hifadhini.

Akizunvumza na wananchi wa vijiji hivyo, Kitandula alisema urejeshaji huo ambao unafanywa kwa kutimia helikopta ni jitihada za makusudi zilizofanywa na serikali katika kuwahakikishia usalama wananchi. "Limelenga na kuboresha uhifadhi kuendelea kuwa endelevu. Urejeshwaji huu wa tembo unatumia gharama kubwa, lakini serikali imejipanga kupunguza kero wanayotana nayo wananchi wa maeneo haya na kuhatarisha usalama wa maisha na mali zao," alisema.

Kiongozi huyo aliagiza taasisi zilizoko chini ya wizara hiyo kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kutatua changamoto hiyo inayochangia madhara kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Adam Malima, alipongeza hatua hiyo akisema kuwa, changamoto ya tembo katika maeneo hayo ni ya muda mrefu.

Mbunge wa Mvomero, Jonas Zeeland, alisema uwezeshaji huo ni faraja kubwa kwa wananchi, kwani wamekuwa wakileta uharibifu mkubwa wa mali na kuhatarisha maisha yao. Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Dk. Eblate Mjingo, alisema taasisi hiyo imeendelea kubuni mbinu mbadala za kutatua changamoto za migongano ya binadamu na wanyamapori hususan tembo, ikiwamo vifaa vilivyotolewa kwa wananchi vya kujikinga vilivyotolewa na wizara hiyo.

# Kliniki ya sheria kwa wanahabari kuzinduliwa Mei

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye, anatarajiwa kuzindua Kliniki ya Sheria kwa Waandishi na Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Mei 3, mwaka huu.

Lengo la kliniki hiyo ni kushughulikia changamoto mbalimbali zinazoikumba sekta ya habari na wafanyakazi wake.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, aliyasema hayo jana Dar es Salaam na kusema uzinduzi huo utafanyika katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani yanayotarajiwa kuadhimishwa Mei 3, mwaka huu, jijini Dodoma.

Matinyi alisema maadhimisho hayo yatakayobebwa na kaulimbiu isemayo "Waandishi wa Habari na Changamoto za Kimazingira" na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Alisema washiriki wengine ni pamoja na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, na zaidi ya wadau 200 kutoka mataifa mbalimbali.

"Madhumuni ya maadhimisho haya ni kupitia kiwango cha uhuru wa vyombo vya habari duniani, kuangalia uandishi wa taarifa za mazingira na mabadiliko ya tabianchi na namna ya kulinda uhuru wa vyombo vya habari.

"Pia maadhimisho haya ni jukwaa muhimu katika kuibua changamoto za kisera na kuangalia namna ya uboreshaji wa mazingira ya sekata hiyo nchini," alisema.

Aliongeza kuwa majadiliano yote yatakayofanyika katika siku hiyo yatachukuliwa na serikali na kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na wadau wa habari kwa kuweka mikakati mahususi ya kuendeleza sekta ya habari.

Rais wa Umoja wa Vyama vya Waandishi wa Habari (UTPC), Deogratius Nsokolo, alisema maadhimisho ni muhimu kwa kuwa yanasaidia kukuza uelewa wa wanahabari kuhusu masuala mbalimbali mtambuka ambayo tasnia ya habari inapaswa kuyasemea.

Alisema yanasaidia pia kuikumbusha jamii kuhusu umuhimu wa kuheshimu uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kutoa na kupata taarifa, pamoja na kuwaleta pamoja waandishi wa habari kufanya tathmini ya vyombo.

Pia alisema yatasaidia kupata fursa ya kuchochea mazungumzo kuhusu majukumu ya wanahabari katika kukuza uwazi, uwajibikaji na demokrasia.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Teknolojia (UNESCO) Tanzania, Michel Toto, alisema maadhimisho hayo ambayo shirika hilo ni sehemu ya washiriki, yanalenga kuona ni kwa kiasi gani wanaendelea kuimarisha mazingira ya waandishi wa habari na kuhakikisha usawa wa kijinsia unazingatiwa.

# Makalla: Nayajua majukumu yangu

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amesema nafasi aliyopewa anafahamu majukumu yake na yeye na wenzake watafanya kazi kubwa iliyokusudiwa kwa weledi na uzoefu kuhakikisha chama kinapata ushindi katika uchaguzi.

Makala aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mapokezi ya Sekretarieti ya CCM Taifa yaliyofanyika katika ofisi ndogo za Lumumba huku akisema wako baadhi wanamkumbusha majukumu yake katika mitandao.

"Ninaposema nimerudi nyumbani naelewa majukumu ya Katibu wa Uenezi na Mafunzo wa CCM maana nasoma mitandaoni baadhi wananikumbusha majukumu, nawaambia nayaelewa kwa kuwa yamo kwenye katiba ya chama Ibara ya 107 kifungu cha pili A hadi F.

"Timu imekamilika na uzuri wa sekretarieti hii tunajuana na bosi wetu tunamheshimu kwa sababu ametuongoza, ametutengeneza. Ingekuwa kuingia jeshini, namba yake inasoma ya kwanza. Tutafanya kazi kwa bidii na kukiletea chama ushindi.

Msingi wa chama chochote cha siasa ni kushika dola na ukitaka ushinde vizuri uchaguzi mkuu lazima upate ushindi mzuri uchaguzi wa serikali za mitaa. Kazi yetu sasa tunarudi kwa wanachama wa kawaida tutalala huko tutapiga kambi lazima kieleweke," alisema.

Makalla amewataka wanachama wa CCM waamini wanae Mwenezi na wasiwe na wasiwasi hawajapangwa kwa bahati mbaya na yupo tayari kwa mdahalo wowote kujibu hoja na kushindana kwa hoja na sio vihoja.

"Nipo tayari kwa mdahalo wowote kujibu hoja bila wasiwasi, nataka kuwaambia upele umepata mkunaji, nipo tayari kwa siasa za maridhiano, tushindane kwa hoja sio kwa vihoja bali kwa hoja nipo tayari,"alisema.

Alisema watafanya kazi kubwa iliyokusudiwa na chama kwa weledi na uzoefu waliokuwa nao kuhakikisha chama kinapata ushindi mkubwa.

"Nimepokea mikoba kutoka kwa mdogo wangu, Paul Makonda, aliyekuwa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha amenikabidhi ofisi, watumishi, makabrasha tunamshukuru na tunaheshimu mchango wake tutaendelea kumpa ushirikiano," alisema Makalla.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Wazazi Tanzania, Ally Hapi, alisema wako tayari kwa mapambano wapinzani kazi yao ni kelele Rais Samia Suluhu Hassan, amewatengenezea mazingira mazuri ingawa hawana shukrani.

"Rais Samia ametengeneza mazingira mazuri wanafanya mikutano, wamefanya shughuli zao na wamepewa ruzuku lakini hawana shukrani niliwasikia wengine wakilalamika katika uchaguzi mdogo wanasema bora hawajatuachia yaani CCM ifanye kazi kuwaachia kata uchaguzi ni kazi," alisema.

# Suluhu malalamiko kuhusu NHIF yaja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema ndani ya wiki moja kuanzia sasa serikali itakuwa imemaliza malalamiko yaliyoko kwa wanachama wanaotumia huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na vituo binafsi vya afya.

Ummy aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo.

"Kuna malalamiko kuhusu bima ya afya na hili niwaambie tutatoboa tu ndugu zangu, kwa hiyo ninaamani ndani ya wiki moja tutakuwa tumemaliza malalamiko yote na misuguano iliyoko," alisema.

Alisema Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya amemwambia kuwa hadi Aprili 10, mwaka huu, watakuwa wamepata ripoti ya Dk. Baghayo Saqware hivyo anaamini maeneo ambayo yana changamoto yatafanyiwa kazi.

"Lazima tuwe na bima iliyo endelevu, lakini hospitali pia, nazo zipate mapato ili waweze kujiendesha na kutoa huduma, pia wanachama wapate huduma wanazozihitaji na ndiyo hoja ya wafanyakazi kupata kile kinacholingana na uchangiaji wao,"alisema Waziri Ummy.

Mtifuano baina ya NHIF na Chama cha Wenye Hospitali Binafsi (APHFTA), ulianza mwezi wa pili mwaka huu baada ya NHIF kutangaza kuanza kwa kitita kipya Machi Mosi.

Wanachama wa APHFTA walitangaza kugoma kutibu wanachama wa NHIF iwapo kitita hicho kipya kitatumika wakisema kuwa kitawafanya wapate hasara na kufunga hospitali zao.

Chama hicho kilisema kuanza kitita hicho kitazifanya hospitali nyingi binafsi kufa kifo cha asili kwani zitashindwa kujiendesha kutokana na kuongezeka kwa gharama za maisha huku gharama za matibabu zikishushwa.

Taarifa ya chama hicho iliyosainiwa na Mwenyekiti wao, Februari 27 mwaka huu, Dk. Egina Makwabe ilisema: "Kitita kilianza kutumika mwaka 2016 na mpaka mwaka huu hakikufanyiwa mabadiliko yoyote licha ya gharama za maisha kuendelea kupanda, leo wanakuja tena kupunguza gharama za huduma badala ya kuongeza wanataka hospitali binafsi zife, badala ya kusaidia sekta binafsi wanataka kuiua," alisema

"Serikali yenyewe haina uwezo wa kuwahudumia wagonjwa wote ndiyo maana imekuwa ikisisitiza ushirikishwaji wa sekta binafsi kupitia PPP lakini mbona wamegeuka tena wanataka kuua hospitali binafsi badala ya kuzisaidia," alihoji kiongozi huyo

NHIF nayo kupitia Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Benard Konga, ilitoa taarifa ikisema kuwa kitita kipya kingeanza kitaanza kutumika Machi Mosi baada ya maoni ya wadau wote kusikilizwa.

Ilisema maboresho ya kitita yalifanyika mwaka 2016 miaka nane iliyopita hivyo kuwa na umuhimu wa kufanya maboresho mapya ikiwemo kuongeza huduma ambazo hazikuwepo kwenye kitita kipya.


# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**COMPANY LTD na MUDU COMPANY LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na Benki ya **INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK (T) LTD,** tutauza kwa minada ya hadhara nyumba/dhamana zifuatazo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe/siku ya tangazo hili. Nyumba/Viwanja hivi zimewekwa rehani kudhamini mikopo iliyotolewa na benki ya ICBTL kwa wakopaji wafuatao.

Pia, Tangazo hili la minada ya hadhara, ni notisi ya siku kumi na nne(14) kwa wakopaji /wadhamini wa mikopo hii kuhusu mauzo ya dhamana zifuatayo kwa minada ya hadhara.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ZITAKAZOUZWA**

| NO | JINA LA MKOPAJI/MDHAMINI | TAARIFA ZA DHAMANA | TAREHE YA MNADA | DALALI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MAFIGOLO GENERAL SUPPLIES (Mkopaji)<br>NAETWE GODFREY MLELE (Mmiliki/Mdhamini)<br>S.L.P 55178 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari: 101460, iliyopo kiwanja na. 2004 ,kitalu'C', MBEZI LUGURUNI,MANISPAA YA UBUNGO,DAR ES SALAAM | 30/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | ORBITER DEBT COLLECTION &AUCTINEERS COMPANY LIMITED<br>TEL NO: 0713751800 |
| 2 | AGNES GABRIEL NTUNGUKA (Mkopaji)<br>ABUBAKAR MUSSA BAGAYA (Mmiliki/Mdhamini)<br>S.L.P 5894 Dar Es salaam | Kiwanja cha makazi chenye hati nambari: 110150, Kiwanja na. 239 Kitalu '17',BUYUNI CHANIKA,MANISPAA YA ILALA , DAR ES SALAAM | 23/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | ORBITER DEBT COLLECTION & AUCTINEERS COMPANY LIMITED<br>TEL NO: 0713751800 |
| 3 | CARGO STAR LIMITED (Mkopaji)<br>LEO JOSEPH MANYARA (Mmiliki/Mdhamini)<br>S.L.P 10000 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari: 84639, iliyopo kiwanja na. 14 ,kitalu'K', UKONGA,MANISPAA YA ILALA,DAR ES SALAAM | 29/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD<br>TEL NO: 0755506970 |
| 4 | DABENCO ENTERPRISES LIMITED (Mkopaji)<br>GODFREY AUGUSTINE MPINGE(Mmiliki/Mdhamini)<br>S.L.P 76164 Dar Es salaam | Kiwanja cha makazi chenye hati nambari: 138799, lililopo kiwanja na. 6 na 8 ,kitalu'D', NIANJEMA,MANISPAA YA BAGAMOYO,DAR ES SALAAM | 26/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | MUDU COMPANY LIMITED<br>TEL NO: 0768672367 |
| 5 | MATESO GROUP COMPANY LIMITED (Mkopaji)<br>PETER ROWLAND LAIMOS (Mmiliki/Mdhamini)<br>S.L.P 19188 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari: 110468, iliopo kiwanja na. 185 ,kitalu na 9, Ilala Buyuni area-Chanika ,DAR ES SALAAM | 24/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | ORBITER DEBT COLLECTION &AUCTINEERS COMPANY LIMITED<br>TEL NO: 0713751800 |
| 6 | LINUS PATRIC KALANDAMWAZYE T/A SICHULA ENTERPRISES (Mkopaji)<br>EVA STEPHEN MHINA (Mmiliki/Mdhamini)<br>S.L.P 111937 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari 84643, iliopo kiwanja na.2046 , ,kitalu' 'B', KIMARA MANISPAA YA UBUNGO ,DAR ES SALAAM | 27/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyik mahala iliko dhamana tajwa | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD<br>TEL NO: 0755506970 |
| 7 | SALOME ANDREW KOMBA T/A SALOME COMMERCIAL CENTRE (Mkopaji)<br>SALOME ANDREW KOMBA<br>S.L.P 60161 Dar Es salaam<br>(Mdahamini/Mmiliki) | Majengo ya makazi na biashara yenye hati nambari: 55928, Kiwanja na. 1030 , Mbezi Tangi bovu kwa komba , Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam | 03/05/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi<br>Mahala: Mnada utafanyika mahala ilipo dhamana tajwa. | MUDU COMPANY LIMITED<br>TEL NO: 0768672367 |

Wanunuzi wote wenye nia na uwezo,mnakaribishwa kuja kukagua nyumba/dhamana kwa vigezo na masharti yafuatayo:

**VIGEZO NA MASHARTI YA MNADA;**

1. Mali/Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 kutokea siku ya mnada.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa na mnada utarudiwa kwa tarehe nyingine.
4. Gharama za kuhamisha umiliki na kumtoa mdaiwa/mpangaji "Eviction" na nyinginezo, zitakuwa juu ya Mnunuzi.
5. Ukaguzi wa dhamana unaweza kufanywa na wanunuzi, siku yoyote kuanzia siku ya tangazo hili kati ya saa tatu asubuhi na saa kumi na moja jioni.
6. Kwa taarifa zaidi,wasiliana na kampuni husika ya uuzaji .

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi ya Twiga Stars fainali CAF yaanze mapema

**WAKATI** mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania unatarajiwa kufanyika kuanzia Aprili 15, mwaka huu, kikosi cha Timu ya Taifa (Twiga Stars), kitaenda kupeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano ya Afrika (WAFCON), hivi karibuni.

Michuano ya WAFCON itafanyika baadaye Juni, mwaka huu huko Morocco na Twiga Stars imekata tiketi ya kushiriki fainali hizo kwa mara ya pili.

Kwa mara ya kwanza Twiga Stars kushiriki fainali hizo zinazoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ilikuwa ni mwaka 2010 jijini Johanesburg, Afrika Kusini na kikosi kilikuwa chini ya nyota wa zamani wa Taifa Stars na Yanga, Boniface Mkwasa 'Master'.

Kuelekea mashindano ya WAFCON mwaka huu, Twiga Stars inahitaji kwenda katika fainali hizo ikiwa imara, kwa maana inakwenda kushindana kusaka rekodi mpya na si kwenda kushiriki au kukamilisha ratiba.

Ili Twiga Stars iende kufanya vizuri katika fainali hizo, Idara ya Ufundi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), inatakiwa iangalie vyema programu za timu hiyo kwa ajili ya maslahi ya nchi.

Inafahamika wazi idadi kubwa ya wachezaji wanaounda kikosi hicho wanatoka katika Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake, na kwa maana hiyo, kama kuna jambo la muhimu la kufanyia kazi wakati mzunguko wa pili wa ligi hiyo unatarajia kuanza, ni vyema likatazamwa kwa umakini.

Wachezaji wanahitaji kuwa na mazingira mazuri katika klabu zao ili baadaye waje kuipa matokeo chanya timu ya taifa, huu ni wakati wa TFF kuongeza na kuimarisha mahusiano na klabu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake kwa ajili ya kuwasaidia kuwa kwenye mazingira rafiki wakati wanashiriki ligi.

Tunahitaji kuona kila kitu kinachohusiana na soka la wanawake kinakwenda vizuri kwa sababu huko ndio maandalizi rasmi ya Twiga Stars yanapoanza, na pale wanapoingia kwenye kambi ya Kocha Mkuu, Bakari Shime, wanakwenda kumalizia na kurekebisha mapungufu machache yaliyobainika.

Ili timu hiyo iende Morocco kwa kujiamini, huu ndio wakati wa TFF, serikali, taasisi, makampuni na wadau mbalimbali wa michezo kuungana kwa vitendo kusaidia maandalizi ya mabinti zetu ambao tunaamini wanaweza kwenda kuiletea heshima Tanzania.


Ni wazi Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeweka fungu kwa ajili ya kuhudumia timu za taifa, lakini ikumbukwe gharama zinazohitajika, na ili kufikia ndoto za kuvuna matokeo chanya, ni lazima michango ya ziada ipatikane kutoka kwa wadau.

Twiga Stars inahitaji kupata kambi yenye ubora pamoja na kutafutiwa michezo ya kirafiki na timu zilizo katika ubora ili kuwajenga wachezaji kwa kuwapa uzoefu wa kucheza mechi ngumu. Mechi hizo si tu zitawapa uzoefu au kuwajenga, lakini zinawaondolea hofu wachezaji wa Twiga Stars pale watakapokwenda kushiriki fainali za WAFCON, wao ni tofauti, nyota watakaokwenda kushiriki fainali za mwaka huu, hakuna hata mmoja ambaye alikuwepo kwenye fainali za mwaka 2010.

Kama ambavyo wanawake wamekuwa wa kwanza kushiriki fainali za Kombe la Dunia (Timu ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 maarufu Serengeti Girls), za U-17 zilizofanyika mwaka juzi huko India na kutolewa kwenye hatua ya robo fainali, tunaamini hata kwa dada zao wanaweza kuweka rekodi ya kufika mbali au kurejea na kikombe cha ubingwa wa Afrika.

Pia huu ndio wakati muhimu kwa wachezaji kujituma kwenye mazoezi ili kuimarisha viwango vyao kwa sababu fainali za WAFCON zitawaweka upya sokoni kwa sababu makocha na mawakala kutoka sehemu mbalimbali watafuatilia michuano hiyo ili kusaka nyota kwa lengo la kwenda kuboresha klabu zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:**
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Championship kuna shida, macho ya ziada yatakiwa

Na Adam Fungamwango

**NILIANDIKA** wiki iliyopita kuwapa angalizo viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) kuhusu mechi zilizobakia za Ligi ya Champioship, zikibaki raundi nne tu kukamilisha msimu wa 2023/2024.

Kwa sasa zimebaki mechi tatu kwa kila timu, huku kukiwa na vita kali ya kupanda kwa KenGold, Pamba FC, Biashara United, Mbeya Kwanza na TMA.

Nikasema wanahitajika waangalizi maalum katika michezo hiyo kwa sababu inawezekana kabisa kukawa na vitendo vya upangaji wa matokeo.

Timu hizi zinazogombea kupanda daraja moja kwa moja, wanacheza na baadhi ya timu ambazo hazina chochote cha kupoteza, haziwezi kupanda daraja, kwenye mechi za mchujo, wala kushuka daraja, hivyo uwezekano huo upo.

Tatizo ni Watanzania kuwa na tabia ya kujisahaulisha, au kuona hili si tatizo kubwa sana.

Kwa bahati mbaya sana huko huko katika Ligi ya Championship ndipo watu wanapokutwa au kukamatwa na tuhuma za upangaji wa matokeo katika soka letu zaidi kuliko kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nasema hivi kwa sababu imeshatokea huko nyuma kesi za upangaji wa matokeo katika mechi za ligi hiyo ambayo zamani iliitwa Ligi Daraja la Kwanza na kupelekea baadhi ya viongozi, makocha na wachezaji kufungiwa.

Katika soka hapa nchini, Ligi ya Championship ndiyo ushahidi wa upangaji wa matokeo umeshawahi kupatikana na wahusika kufungiwa, si mara moja wala mbili.

Binafsi mechi mbili zilizochezwa bado zinaniumiza kichwa.

Nilipoandika tu makala ile, kesho yake, Pamba FC ikaikung'uta Polisi Tanzania mabao 5-1, kesho yake Biashara United ikalipiza kwa kuwabamiza Transit Camp mabao 5-1.

Sisemi kama timu hizo zote zimepanga matokeo, lakini kama mimi ningekuwa mhusika ningeanzisha uchunguzi, potelea mbali baadaye ionekene hakuna ukweli wowote, ni mpira tu.

Kwa wale watu wenye utaalam wa intelejensia, hapa lazima watakuwa na maswali kadhaa ya kujiuliza.

Ni kwa nini Pamba imeshinda mabao 5-1? Ni kwa nini kesho yake Biashara United ikashinda idadi hiyo hiyo ya mabao? Kwa nini timu zilizoshinda idadi hiyo ya mabao ni zile zinazofuatana katika msimamo wa ligi na si zingine?

Ikumbukwe kuwa Pamba FC ipo nafasi ya pili kwa pointi 58 na Biashara United ya tatu kwa pointi 56, kama ilivyo Mbeya Kwanza. Biashara United ipo juu ikiwa na mabao 52, Mbeya Kwanza ya nne ikiwa na mabao 44. Je matokeo yanayotokea sasa siyo ya kimkakati? Je timu zinatafuta mabao mengi kwa sasa ili yawasaidie baadaye?

Haya maswali yanaweza kabisa kufanya wahusika kupeleka waangalizi kwenye mechi zilizobaki ambapo kila timu imebakisha mechi tatu.

Tukiacha hilo, maamuzi ya Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi na Bodi ya Ligi yaliyotoka juzi, katika kikao chake cha Aprili 3, mwaka huu yanaonyesha kabisa kuna matatizo makubwa kwenye ligi hiyo yanayohitaji uangalizi wa hali ya juu.

Kwa sababu mbali na kupanga matokeo, kuna ubabe wa hali juu, utovu wa nidhamu, pamoja na upendeleo.

KenGold imetozwa faini kwa kukataa kutumia chumba maalum dhidi ya Pamba, baadhi ya wachezaji kujisaidia haja ndogo kwenye kona za uwanja, mchezaji mmoja wa Pamba, Mudathir Abdullah, kumpiga ngumi mwamuzi na akapiga teke mlango wa kuingilia katika vyumba vya kubadilishia nguo, na adhabu zinazotokana na vituko vingi kama kurusha mawe, wachezaji kuvamia waamuzi, inaonyesha kuna matatizo makubwa kwenye ligi hiyo.

Naishauri TFF katika mechi zilizobaki iwe makini, kwa sababu kuna viashiria vingine, mbali na vya kupanga matokeo, lakini kuzuka vurugu kubwa kama hakutakuwa na usimamizi mzuri na madhubuti.

## HABARI KITAIFA



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika, Wasia Mushi, akizungumza wakati wa futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JKCI yafanya upasuaji wa tundu kurekebisha mishipa iliyotanuka

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), imefanya upasuaji wa tundu dogo kurekebisha mishipa ya damu iliyotanuka na kupasuka kwa wagonjwa watano, hivyo kuokoa Sh. milioni 750.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema hayo juzi kuwa matibabu hayo yamekuja baada ya serikali kuipatia taasisi hiyo takribani Sh. milioni 900 huku akibainisha kwamba kuna wagonjwa wapatao 30 wakisubiri matibabu kama hayo.

Alisema tatizo hilo huwakumba watu wengi ambao baadhi yao walipougua walianguka ghafla na kupoteza maisha na awali ililazimika kutibiwa nje, hasa India.

"JKCI kwa kushirikiana na wenzetu kutoka Mumbai, India, kutoka hospitali ya Astra, tutawafanyia huduma hii wagonjwa watano. Mmoja tayari kafanyiwa na wengine wataendelea.

"Hawa watano huduma kwa mtu mmoja inagharimu takribani Sh. milioni 80 nchini. Ukienda India kwa mgonjwa mmoja, nauli na wanaomsindikiza ingegharimu Sh. milioni 150," alisema Dk. Kisenge.

Bingwa huyo wa moyo, alisema tatizo la mishipa kupata hitilafu hutokana na shinikizo kubwa la damu, matumizi ya sigara, unywaji pombe na unene uliokithiri.

"Kuna tatizo kubwa kati ya wagonjwa 100 ukiwaona kliniki unaweza kukuta mmoja au wawili wana tatizo hili, kwa hiyo lipo. Tuna wagonjwa 30, wanaosubiri matibabu, hapo hatujaemda mikoani.

Dk. Kisenge alisema huduma hiyo ni ya kwanza na inayotolewa Tanzania pekee kwa nchi za Afrika Mashariki na kwamba wanaougua wafike katika taasisi hiyo kwa matibabu.

Alisema huo ni upasuaji uliofanyika kwa mara ya kwanza nchini ukitumia mtambo wa 'Cathlab' kupitia tundu dogo.

Mkurugenzi wa Upasuaji wa JKCI, Dk. Angela Muhozya, alisema upasuaji huo ni hatari kubwa katika kufungua kifua kuliko huduma ya tundu dogo na ni muhimu kumhudumia mgonjwa kabla ya mshipa haujapasuka.

"Kuna mshipa unapandikizwa baada ya kufanya vipimo, kwenye mshipa pale palipo na tatizo. Wataalamu wetu wanafundishwa kufanya huduma hii," alisema Dk. Muhozya.

Bingwa wa Upasuaji wa Moyo katika taasisi hiyo, Dk. Alex Joseph, alisema mmoja wagonjwa aliyefanyiwa upasuaji ana umri wa miaka 66 na ilitumia saa mbili.

Alisema mgonjwa huyo, mshipa mmoja unaopita kwenye tumbo ulitanuka na anaendelea vizuri, akianzia chumba cha uangalizi maalum (ICU) kisha atahamishiwa wodi ya kawaida.

Naye Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka India, Dk. Gireesh Warawdekar, alisema huduma hiyo ya tundu dogo hupunguza hatari ya kifo kwa mgonjwa, na pia upasuaji huo wa kukarabati mishipa ya damu iliyotanuka sehemu ya kifua na tumbo kwa kutumia kifaa maalumu (stent).

Ali Amour Suleiman, mkazi wa visiwani Zanzibar, ambaye amefanyiwa upasuaji huo, alisema alibainika na tatizo katika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja.

"Nilibainika mshipa wangu mkubwa wa damu unaotelemka kutoka kwenye moyo kuja sehemu ya chini. Nilipewa rufani kuja JKCI. Nimefika hapa tangu Januari na sasa Aprili hii ndiyo nimefanyiwa upasuaji," alisema Ali.

## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTLINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI | ZACHARIA ANTHONY KAPAMA | KIFURU KINYEREZI-ILALA | 17/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA 2.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 3. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2.SALUM JUMA MARWA 3.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.MBEZI MANYEMA 2.KIGOGO KATI 3.KINZUDI GOBA | 9/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MTONDI SIAGI KICHELE | NYUMBA | KURUTHUMU ABDALLAH NYAMKO | NYAKATO -MWANZA | 22/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 15/04/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 16/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.IGELEGELE BUGARIKA 2. BUJINGWA-MWANZA | 09/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 15/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 09/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 17/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 18/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | KIGODA ABBASI KIGODA | NYUMBA | KIGODA ABBASI KIGODA | VIGWAZA | 09/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA | MPOKI BROWN MWAIPASI | KILUVYA | 22/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | NICHOLAUS DEOGRATIUS MUHAGAMA | NYUMBA | ANNA MANYANGU MADUHU | NKUHUNGU DODOMA | 22/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | AISHA HAMADI KIVINA | NYUMBA | AISHA HAMADI KIVINA | KIVULE MAJOHE | 22/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | JOYCE GENES SHIRIMA | NYUMBA | FRIDA ELIESKIA FUE | HONDOGO KIBAMBA | 15/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 15/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | OWDEN MKUMBALA NYONDO | NYUMBA | OWDEN MKUMBALA NYONDO | ISYESYE-MBEYA | 16/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 17/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 18/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA | KASSIAN ANTHON NINDI | TABATA KISUKULU | 23/04/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | NYUMBA (2) | 1.HASSAN RAMADHANI HARASHI 2.HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | 1.YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE 2.TAMBANI MKURANGA | 23/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | ANNANEEMA DANIEL RITTE | KIWANJA | ANNANEEMA DANIEL RITTE | SEGU CHINI, KATA YA NALA - DODOMA | 09/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | UPENDO JACKSON LEMA | NYUMBA | EUNICE BOSWELL TARATINU | KIMARA | 17 /04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea (MARUDIO) |
| TEGETA | MUSSA MATHIAS SHIJA | NYUMBA | MUSSA MATHIAS SHIJA | UDINDIVU- BAGAMOYO | 22/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea (MARUDIO) |
| UBUNGO | LISTER BENEDICT CHIMYA | NYUMBA | LISTER BENEDICT CHIMYA | KIMARA | 18/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea (MARUDIO) |
| UBUNGO | MKONDA HOUSE OF FOOD | NYUMBA | PAMELA MACILA NYITAMBE | TABATA-KIMANGA | 19/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | OSCAR JACKSON SEME | NYUMBA | OSCAR JACKSON SEME | MSAKUZI KUSINI | 22/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea |
| TEGETA | FATUMA BAKARI BENDERA | NYUMBA | FATUMA BAKARI BENDERA | KIMELE-VIKAWE | 24/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea |
| UBUNGO | MUSSA INANO CHACHA | NYUMBA | HABIBU MUSSA MACHOROKO | MBAGALA KWA NYOKA | 25 /04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea |
| TEMEKE | FOCUS JOSEPH KICHINDA | NYUMBA | FOCUS JOSEPH KICHINDA | MJI MPYA-KIMARA | 26/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea |
| AGGREY | SYLIVESTER APOLINARY MBOYA | NYUMBA | SYLIVESTER APOLINARY MBOYA | MBEZI MSUMI | 29/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea |
| AGGREY | OMARY SAIDI OMARY | NYUMBA | MIZE MASOUD HASSANI | MIKWAMBE | 29/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea |
| UBUNGO | ALLY SHAWEJI OMARY | NYUMBA | ALLY SHAWEJI OMARY | KIBAMBA | 26/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea (MARUDIO) |
| TEGETA | YOHANA BRUNO SHAYO | NYUMBA | WILSON ELICHILIA MBOYA | KEREGE-BAGAMOYO | 17/04/2024 saa 4 asubuhi na kuendelea (MARUDIO) |
| TEMEKE | SALIM SULEIMAN HEMED | KIWANJA | SALIM SULEIMAN HEMED | MKURANGA | 16/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715868000/0714939933/0785242219/0759282344/0787129539/0767808848/0754497396/0678799566/0655715138/0759648448

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# Wakulima wapewe elimu matumizi kuhusu stakabadhi ghalani

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKUU wa Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, Kemirembe Lwota, amewaagiza wataalam na viongozi wa vyama vya ushirika wilayani humo kuelimisha wakulima kuhusu matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

Amesema lengo ni ili kunufaika na uuzaji wa mazao yao kwa bei nzuri na ya uhakika.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani iliyofanyika Kata ya Heka, mkoani hapa, alisema elimu hiyo ni kwa manufaa yao.

"Ninawaomba sana viongozi wa vyama hivi vya ushirika pamoja na wataalamu wetu, kuendelea kutoa elimu kwa wakulima wetu kuhusu matumizi ya mfumo huu wa stakabadhi ghalani, kwani ni kwa manufaa yao," alisema.

Lwota alisema mfumo huo serikali imeuanzisha ili mkulima apeleke mazao yake ghalani, lengo ni kuongeza thamani na mkulima kupata bei inayoendana na jasho la uzalishaji.

"Wito wangu kwa wakulima ni kuhakikisha mnazingatia mwongozo uliotolewa na serikali kuhusu mfumo huuambao ni kwa manufaa yenu na utawasaidia kuboresha maisha yenu," alisisitiza.

Pia aliwataka kusimamia mfumo huu kwa ufanisi na kuhakikisha wakulima wanalipwa fedha zao kwa wakati na kutatua malalamiko yanayojitokeza.

"Ndugu zangu lazima tujue kuwa, tunapaswa kuongeza uzalishaji katika kilimo chetu kwa kuhakikisha tunatumia mbolea ya kutosha wakati wa kulima," alisema.

# ATCL yajipanga kuelekea kujitegemea

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, amesema hadi sasa serikali imewekeza zaidi ya Sh. trilioni 2.4 kwa ajili ya kuliendeleza na kukuza Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Aidha, amesema kuna matokeo na manufaa makubwa kufuatia uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika kampuni hiyo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi aliyetaka kujua mafanikio ya uwekezaji kwneye kampuni hiyo, alisema moja ya matokeo hayo ni kwamba kwa hivi sasa ATCL haitegemei ruzuku ya serikali kulipia mishahara, matengenezo ya ndege na kununulia mafuta ya ndege kabla ilivyokuwa miaka michache huko nyuma.

Hadi sasa, alisema serikali imewekeza takribani shilingi trilioni 2.4 katika ununuzi wa ndege, ujenzi wa miundombinu wezeshi ya ATCL katika biashara ya usafiri wa anga pamoja na ulipaji wa sehemu ya madeni yaliyolimbikizwa.

"Kutokana na uwekezaji huo, ATCL imeongeza idadi ya ndege kutoka moja mwaka 2016 hadi 15. Mtandao huu umewezesha kuunganisha safari za ndani, kikanda na kimataifa," alisema.

Pia alisema manufaa mengine ni katika ajira ambapo uwekezaji ATCL umezalisha nafasi za kazi kutoka 171 mwaka 2016 hadi ajira 780 kwa sasa mwaka 2024.

Pia alisema ATCL imechangia katika kuongeza fedha za kigeni kutoka Dola za Marekani milioni 43.36 mwaka 2021/2022 hadi Dola za Marekani milioni 79.22 kwa 2022/23. Prof. Kahyarara alisema mchango wa ATCL kwenye kodi, ada na tozo za kisheria umeongezeka kutoka Sh. bilioni 28.6 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 66.7 mwaka 2022/23.

Katibu mkuu huyo alisema uwekezaji huo umeongeza sana uwezo wa shirika katika kusafirisha abiria kutoka 106,138 mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia abiria 1,070,734 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Mkakati wa serikali ni kufikisha ndege 19 mwaka 2025 na kuifanya ATCL kati ya Mashirika Makubwa ya Ndege katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).




Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, mkoani Pwani, Meja Edward Gowele (wa tatu kushoto), akikabidhi mtungi wa gesi ya Oryx kwa Furaha Mawikia wakati wa hafla ya kukabidhi mitungi ya gesi na majiko yake 400 kwa wanawake wa vijiji vya Mwalusembe, Kinene, Kitomondo na Kisele wilayani humo juzi. Wanaoshuhudia ni Balozi wa Heshima Shelisheli nchini Tanzania, Maryvyonne Pool (watatu kulia), Meneja Usalama, Afya na Mazingira wa Oryx Energies Tanzania, Janet Mutashobya (wa pili kulia) na Katibu Tawala Wilaya ya Mkuranga, Omary Mwanga (wa pili kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kina maji Bahari ya Hindi ukanda wa Tanzania chaongezeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imekiri kina cha maji ya Bahari ya Hindi ukanda wa Tanzania kimeongezeka kutokana na kuendelea kupanda kwa joto la dunia linalosababisha kuyeyuka kwa barafu katika maeneo mbalimbali ya duniani.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kuna ukweli kwamba kina cha maji ya Bahari ya Hindi ukanda huu kimeongezeka kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kuhoji nini athari zake.

Akijibu swali hilo, Dk. Jafo alisema kwa mujibu wa utafiti na vipimo vilivyoko, maji ya Bahari ya Hindi katika Pwani ya Dar es Salaam yanaongezeka kwa wastani wa kiasi cha milimita sita kwa mwaka tangu mwaka 2002.

Alitaja athari za kuongezeka kwa kiwango cha maji ya bahari kuwa ni pamoja na; kuongezeka kwa mmomonyoko na upotevu za fukwe, uharibifu wa miundombinu kama vile gati za bandari, barabara, nyumba ofisi na masoko.

Pia alisema kunasababisha upotevu wa bioanuwai muhimu ikiwamo mikoko na nyasi bahari, upotevu wa ardhi ya kilimo na makazi, na visima vya maji baridi kuingiwa na maji ya chumvi na mafuriko ya mara kwa mara. Katika swali la nyongeza, Prof. Ndakidemi alisema kwa kuwa serikali imekiri kuwapo ongezeo la kina cha maji katika Bahari ya Hindi, nini mpango wa serikali wa kulinda maeneo hayo ili yasije kuzama kwenye maji siku za mbeleni. Mbunge huyo alihoji serikali inashirikiana vipi na wadau wa kitaifa katika kushughulikia changamoto hiyo.

Dk. Jafo alisema mwaka 2021, serikali ilifanya rejea ya sheria na sera ya mazingira na mpango mkakati wa kushughulikia mazingira, na kuwa sasa inakuja na Sera mpya ya Uchumi wa Buluu ambayo pamoja na mambo mengine itahusika kulinda fukwe zote za bahari. Pia alisema serikali imekuwa na mashirikiano mazuri na wadau mbalimbali wa kimataifa wakiwamo Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) na iko katika mchakato wa kujiunga na shirika linalojihusisha na mazingira kutoka Korea.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum, Asia Halamga (CCM), alitaka kujua mpango wa serikali wa kuokoa Ziwa Babati.

Akijibu swali hilo, Dk. Jafo alisema serikali inakuja na mpango wa bajeti kwa ajili ya kushughulikia magugumaji kwa Ziwa Babati na Ziwa Jipe.

# Kambi ya madaktari yawafikia watu 600

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KAMBI ya madaktari bigwa iliyofanyika jijini Dodoma kwa siku moja, imewafikia zaidi ya watu 600 na kuwapatia huduma mbalimbali za vipimo na matibabu ya kibingwa.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri, juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea na kukagua shughuli mbalimbali za kambi hiyo.

"Serikali tuna kila sababu ya kuwashukuru madaktari bingwa walioamua kuendesha kambi za tiba za kibingwa kwa kuwafuata wananchi hao na kuwapatia huduma bure bila gharama yoyote katika kipindi hiki cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani," alisema.

Alisema madaktari hao wamesaidia kupunguza kero nyingi za wananchi kufuata matibabu mbali na maeneo yao pamoja rasilimali fedha jambo ambalo linaawafanya kushindwa kufika kwa wakati na kupata huduma.

Pia aliitaka jamii kuwa na utaratibu wa kujitoa ili kuwasaidia wengine wasiojiweza ambapo ni ibada iliyo njema mbele za Mwenyezi Mungu kufanya matendo ya huruma.

"Ukifanikiwa kumsaidia muhitaji unakuwa umemgusa mwenyezi Mungu mwenyewe hivyo tuwe na desturi ya kufanya matendo ya huruma ndugu zangu," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya akizungumza na wananchi kwenye kambi hiyo ya madaktarii bingwa, aliwataka kuendelea kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan ili atimize lengo la kuwapatia bima ya afya kwa watu wote.

Naye Mwenyekiti wa kambi hiyo, Dk,Abdalah Baja, alisema madaktari hao bingwa wameamua kutoa huduma bure kwa wananchi ikiwa ni sehemu yao ya sadaka kwa Mwenyezi Mungu.

Dk. Baja alisema ni jambo muhimu kujitoa kufanya matendo hayo ya huruma ili kuwasaidia wananchi wenye changamoto bila kutarajia kupokea chochote kutoka kwao.

# Mahakama yakabiliwa uhaba watumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel, amesema Mahakama ina uhitaji wa zaidi ya watumishi 10,000 huku walioopo wakiwa ni 5,880 ambao wanatumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kukabiliana na hali hiyo.

Pia amesema katika miaka 60 ya Muungano, tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, idadi ya majaji wa Mahakama ya Rufani imeongezeka kutoka 16 hadi 35 ikiwa ni zaidi ya asilimia 100.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Prof. Elisante alisema matumizi ya TEHAMA yamesaidia kwa kiwango kikubwa kuziba upungufu huo.

"Pia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi wanatusaidia kupata watumishi na wiki ijayo, tunatarajia kutangaza matokeo ya usaili uliofanyika wiki mbili zilizopita na usaili wetu ni wa TEHAMA. Hatukusanyi watu wanafanya kwa njia ya mtandao na kupata majibu papo hapo," alisema. Kuhusu Mahakama ya Rufani, mtendaji huyo alisema ongezeko la majaji limekwenda sambamba na uanzishwaji wa masjala ndogo ya mahakama hiyo. "Ongezeko la majaji wa Mahakama ya Rufani kwa sasa linawezesha majopo 11 ya majaji watatu, majopo saba ya majaji watano na majopo matano ya majaji saba kuendesha vikao vya mahakama kwa wakati mmoja,"alisema

Alisema idadi ya vituo vya kusikilizia mashauri ya Mahakama ya Rufani imeongezeka na kutoka 16 hadi 18.

"Vituo vya usikilizaji wa mashauri ya Mahakama ya Rufani viko katika Masjala za Mahakama Kuu za Arusha, Dar es Salaam, Bukoba, Dodoma, Iringa, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Moshi, Musoma, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Songea, Sumbawanga, Tabora, Tanga na Zanzibar," alisema.

Alibainisha kuwa kumekuwapo na faida zilizotokana na kuongezeka kwa majaji wa Mahakama ya Rufani kumepunguza mrundikano wa mashauri, kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi katika masjala zote za Mahakama Kuu, mashauri kusajiliwa na kuamliwa kwa wakati.

Pia alisema ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki Pemba utaanza hivi karibuni na ni miongoni mwa mafanikio yanayolenga kusongeza huduma za utopaji haki karibu na wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (kulia aliyevaa kofia), akimsaidia mtoto kuchunguzwa macho yake na mmoja wa madaktari (kushoto), waliotoka hospitali mbalimbali za Jiji la Dodoma, kwenye kambi ya siku moja ya upimaji wa afya bure katika kata ya Mpunguzi, jijini humo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Uingereza yafungua ofisi ubalozi Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI ya Uingereza imefungua rasmi ofisi ya ubalozi jijini Dodoma na kuzindua mikakati mipya kwa madhumuni ya kuboresha uwekezaji nchini Tanzania.

Uzinduzi huo ulifanyika jana jijini Dodoma na kushuhudiwa na Waziri wa Maendeleo kwa Afrika wa Uingereza, Andrew Mitchell, Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar.

Akizungumza wakati wa ufunguzi, Waziri Mitchell alisema ofisi hiyo ni miongoni mwa majengo ya kidiplomasia ya kwanza kufunguliwa katika mji mkuu wa Tanzania.

Alisema ufunguzi wa ofisi hiyo unaashiria hatua muhimu katika uhusiano kati ya Uingireza na Tanzania.

"Kwa kutambua umuhimu wa kuwa mjini Dodoma, ofisi hii itawezesha kufanya kazi kwa ukaribu kati ya serikali ya Uingereza na Tanzania na pia wadau wengi kutoka nchi zote mbili.

"Siku ya leo (jana) ni ishara ya imani na thamani tunayoweka katika ushirikiano wetu na serikali ya Tanzania, pia ni matokeo ya uhusiano muhimu na wakudumu kati ya watu wa mataifa mawili yenye ushirikiano na urafiki katika ngazi zote," alisema

Aidha, katika hafla hiyo ya uzinduzi huo alitangaza ushirikiano na mikakati mipya ya serikali ya Uingereza na Tanzania ili kukuza maendeleo katika sekta za afya,uwekezaji wa kijamii na ukuaji wa uchumi jumuishi nchini.

Alisema ahadi ya Uingireza ni kuwekeza kwenye kukuza ushirikiano wa ufanisi wa pamoja unaolenga kufungua uwekezaji na biashara kupitia ukuaji endelevu na uundaji wa kazi.

"Ubia huo unalenga kufungua hadi dola bilioni 1.26 za uwekezaji unaofadhiliwa na serikali ya Uingereza nchini Tanzania pia kukuza biashara kati ya mataifa hayo mawili kwa dola milioni 1.26 na kuhamasisha uwekezaji wa kibinafsi kwa dola milioni 1.26 katika biashra ndogo na za kati (SME) za Tanzania," alisema.

Pia alisema dola milioni 18.9 zitatumika kuimarisha mifumo ya afya kufanya kazi na serikali ya Tanzania kuimarisha ustahimilivu wa huduma za afya,kupunguza vifo vitokanavyoweza kuzuilika na kukabilina na magonjwa ya mlipuko.

"Dola milioni 15 zitasaidia ushirikiano kwenye haki za afya ya uzazi na jinsia ufadhili huo utawezesha programu iliyopo kurefushwa na kutoa huduma na kuwafikia watu takribani 900,000 ili kupata huduma za uzazi wa mpango zenye ubora wa juu," alisema.

Kadhalika, alisema ahadi ya serikali ya Uingereza ni kuendelea kusaidia mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) ambao hutoa ruzuku kwa asilimia 15 kwa kaya maskini zaidi katika mikoa yote nchini.

Pia alisema dola milioni 6.9 zitasaidia miradi ya mabadiliko tabianchi na mazingira nchini ufadhili amabo utaendelea hadi 2026 na utakuza teknolojia safi za kupika,upatikanaji wa nishati safi na ustahimilivu wa mijini.

Naye Waziri Makamba alipongeza serikali ya Uingereza kwa kuwa moja ya nchi ambazo zimeweka ofisi zake za ubalozi katika makao makuu ya serikali ya Tanzania.

"Serikali yetu baada ya kuanza mchakato wa kuhamisha makao makuu yake kutoka Dar es Saalam kuja hapa Dodoma ilitoa maelekezo kwa ofisi za wizara pamoja na ofisi za Ubalozi kuhamia Dodoma na leo hii tunashuhudia wenzetu wa Uingereza wamehamia hapa rasmi," alisema Makamba

Alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato, ili kuwezesha ofisi za Ubalozi kuhamia makao makuu ya serikali.



# Duka lafungwa madai kuuza pombe Ramadhani

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limethibitisha kufungwa kwa duka la vileo maarufu la kampuni ya ZMMI, visiwani hapa, kwa madai ya kuuza pombe kipindi cha mfungo wa Mwezi wa Ramadhani.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari makao makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar, Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Zubeir Chembera, alisema duka hilo limefungwa na Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar Aprili 2, mwaka huu.

"Maofisa ya Bodi ya Udhibiti Vileo Zanzibar wakiwa katika shughuli zao za kawaida, walifika dukani hapo kutokana na kupata taarifa kwamba wamiliki wa duka hilo wanakiuka sheria ya udhibiti wa vileo. Walipofika wakati wa mahojiano kati ya maofisa hao na wafanyakazi wa duka hilo, kukatokea kutoelewana na kurushiana maneno," alisema. Alisema kutokana na sitofahamu hiyo, maofisa wa bodi hiyo waliwataka wafanyakazi kufunga duka na kuondoka nao kwenda kwenye ofisi za bodi kwa majadiliano.

Kwa mujibu wa sheria ya bodi ya vileo, alisema baada ya majadiliano wahusika walitakiwa kulipa faini na kutakiwa kutekeleza adhabu waliyopewa.

Hata hivyo, alisema baada ya kutokea tukio hilo, kuna taarifa ilienea kupitia mitandao ya kijamii kuwa wafanyakazi watatu wa duka hilo walitekwa nyara na watu wasiojulikana na kutakiwa kufunga duka jambo ambalo si sahihi.

"Baada ya kusambaa kwa taarifa hizo, tulifuatilia kwenye vituo vyote vya polisi Zanzibar na kugundua kuwa hakuna taarifa kama hiyo iliyoripotiwa kinyume cha taarifa zilizokuwa zimetolewa na mtandao mmoja wa kijamii," alisema.

Alipoulizwa kuhusiana na tukio hilo, Katibu wa Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar, Zainab Sururu, alisema atafutwe Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Issa mahfoudh, ndiye mzungumzaji wa suala hilo.

"Mimi nilikuwa katika sherehe za kuwasha mwenge nimerudi Zanzibar. Bado sijazipata vizuri taarifa hizo na muda huu nakwenda katika kikao. Naomba nipe muda wa kuzungumzia suala hilo" alisema Mahfoudh.

Wakati hayo yakitokea, kuna baadhi ya baa karibu tano zinazomilikiwa na taasisi nyeti katika maeneo ya Maisara, Chukwani, Migombani, Mombasa na Ubago, zinatoa huduma za vileo na vyakula tangu kuanza kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Taarifa kutoka katika eneo la tukio, mtaa wa Migombani, zinasema wafanyakazi hao wa ZMMI baada ya kutoka katika ofisi za bodi, pia walifungua malalamiko yao katika kituo cha polisi Mwembe Madema, mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na kupewa RB namba 1390-2024 ya kuvamiwa wakiwa kazini.

Duka la ZMMI limekuwa likitoa huduma za vileo katika kipindi cha Ramadhani kila mwaka na kuwa kimbilio kubwa kwa wawekezaji katika hoteli za kitalii kwenye maeneo mbalimbali ya Unguja.



Rais wa Zanzibar Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na viongozi na wageni waalikwa baada ya kumalizika kwa hafla ya futari maalum iliyoandaliwa na Ubalozi Mdogo wa Oman Zanzibar, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja juzi. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi: Tutazienzi fikra, falsafa za Karume

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wananchi kuzienzi na kuziendeleza fikra na falsafa za kimaendeleo na kizalendo za Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, kwa maslahi ya taifa.

Aliyasema hayo jana katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, katika Kongamano la Sita la Kumbukumbu ya Karume lililofanyika katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kampasi ya Karume, Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema Mzee Karume alijenga upendo na umoja wa kitaifa, misingi bora ya kiuchumi, kuleta haki na kupambana na dhuluma dhidi ya wanyonge, hivyo kumuenzi kwa vitendo kama wanavyothamini Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema kutimia kwa miaka 52 ya kumbukizi ya Mzee Karume ni vyema kujikumbusha misingi ya utendaji wenye kuacha alama katika maisha na mifumo katika serikali kwa kuendeleza na kukuza uzalendo miongoni mwao.

Pia alisema kupitia kongamano hilo, ni vyema jamii ikakumbuka na kurejea katika misingi ya falsafa za uwazi, uadilifu, ushirikishwaji, amani, upendo na ubunifu na utendaji wenye kuboresha maisha ya wananchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alisema Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinamuenzi kwa vitendo Hayati Mzee Karume kila mwaka kwa kufanya kongamano ambalo linatoa fursa kwa wananchi hasa vijana kuzifahamu fikra na falsafa zake.

Alisema kazi kubwa iliyofanywa na Hayati Karume ni pamoja na kuikomboa Zanzibar na kuiweka huru sambamba na kukubali kufanyika kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa taifa la Tanzania, hivyo kuwafanya Watanzania kuwa wamoja hadi sasa.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Steophen Wasira, alisema ni vigumu kuizungumzia Zanzibar pasipo kumtaja Mzee Karume ambaye ndiye aliyeipigania Zanzibar na kuiweka huru kutoka katika makucha ya wakoloni.

Alisema kuwa kuna kila sababu ya kuendelea kumkumbuka Hayati Mzee Karume kwa mema aliyowatendea Watanzania ikiwa ni pamoja na kupigania haki na usawa, kuondosha dhuluma, ubaguzi na matabaka ya makabila na udini na kuwafanya watu wote wawe wamoja na wenye haki sawa.

Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema Ddra ya Chuo hicho ni kuwa kitovu cha utoaji wa elimu bora yenye uvumbuzi na kuendeleza thamani ya umoja wa Kitaifa.

Alisema chuo hicho kupitia Kampasi ya Karume, kitaendelea kuenzi mchango wa Hayati Mzee karume kupitia njia mbalimbali ikiwamo ya makongamano ya kujikumbusha misingi aliyoijenga hasa katika kuimarisha uchumi wa nchi.

## Wezi wadaiwa kuhujumu mradi mkubwa wa maji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU wasiojulikana wameiba nyaya za umeme za usambazaji maji katika mradi wa kisima kikubwa Kwarara Kidutani, wilaya ya Magharibi B, Unguja.

Akizungumza baada ya kufanya ziara jana katika maeneo hayo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini Joseph Kilangi, alisema uharibifu huo hauvumiliki na umerudisha nyuma maendeleo ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi.

Kilango alisema uharibifu huo umesababisha hasara ya Sh. milioni 60 na utafanya mradi huo uchelewe kukamilika. Pia alisema uharibifu huo utasababisha visima tisa kushindwa kusambaza maji kwa sababu ya kukosa umeme.

Katibu mkuu huyo alisema hivi karibuni mradi huo ulitakiwa kukabidhiwa kwa serikali ili kuanza kutoa huduma kwa wananchi lakini kutokana na changamoto hiyo, utachelewa na kutokufikia lengo la serikali.

Alisema kuwa zaidi ya mita 500 za nyaya za umeme katika kisima hicho zimeibwa na kuitia hasara serikali kwa kulazimika kununua nyaya zingine ili kukamilisha mradi huo.

Mradi huo wa kisima cha maji, alisema ni mkopo kutoka benki ya Exim ya India na serikali ndiyo inaolipa, hivyo si vyema kwa baadhi ya wananchi wanafanya uharibifu huo.

Alisema jitihada za serikali ni kuwapatia huduma za maji safi na salama wananchi wote lakini anapotekea mtu kufanya kinyume cha utaratubu, ni kurudisha nyuma jitihada za serikali.

Kilango alisema serikali ya Zanzibar kupitia wizara hiyo, inalaani kwa nguvu zote kitendo hicho na kuviomba vyombo vya dola kufanya uchunguzi kwa wanunuzi wa vyuma chakavu ili kuwabaini waliofanya uharibifu huo.

Wananchi wanaoishi karibu na eneo hilo walisema kitendo hicho cha kuibwa nyaya hizo ni kurudisha nyuma maendeleo ya Zanzibar na wananchi wake, hivyo wameiomba serikali kufanya msako ili kuwakamata wahusika.

Hussen Haji, mmoja wa wananchi hao, alisema wananchi wa maeneo hayo walikuwa wanakabiliwa na ukosefu wa maji safi na salama na walipoona mradi uko mwishoni kukamilika, walipata Faraja lakini wizi wa nyaya umerudisha nyuma matumaini ya kupata huduma hiyo kwa wakati.



**SWIFT**

UKURASA 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE







# HAPA KAYATIMBA KIAINA

RAPA maarufu nchini, Rosa Ree, ameibua mjadala kufuatia kujifananisha na mkongwe wa muziki wa ragggae kutoka Jamaica, Bob Marley.

Mapema wiki hii, kupitia ukurasa wake wa Instagram, Rosa Ree, alijifananisha na mwanamuziki huyo anayependwa duniani kwa kueleza kuna mtu alimwambia kuwa yeye ni Bob Marley wa kizazi cha sasa kutokana na kiwango anachokionyesha katika muziki wake.

"Kuna mtu alisema Rosa Ree ni Bob Marley wa kizazi hiki, nilihisi hivyo," amesema Rosa Ree.

Hata hivyo, baadhi ya watu wameitafsiri kauli hiyo kama kujiinua kupita kiasi kwa mwanamuziki huyo wa kike anayetamba katika hiphp hapa Tanzania.

Baadhi wamesema kuwa kwa sasa Rosa Ree, ni kama ameshuka kisanii kutokana na nyimbo zake kutosikika sana kama ilivyokuwa huko nyuma, hivyo ni kumkosea heshima Bob Marley, ambaye licha ya kufariki nyimbo zake bado zinaendelea kutamba.

"Pengine alitaka kujiinua kwa kujifananisha na mkwengwe huyu anayeheshimika duniani, ni vigumu kwa Rosa Ree kukaa karibu yake hata kwa uimbaji pekee," John Shekevua katika maoni yake.

Hata hivyo, kuna baadhi ya mashabiki wake wamempongeza mwanamuziki huyo na kumtaka kuweka umakini katika kazi zake ili aendelee kusimama katika tasnia ya muziki.

BASI SAWA

## Japhet Zabron kuileta hii...



MWIMBAJI na mwalimu wa kundi la Zabron Singers, Japhet Zabron amesema wimbo wake mpya unaoitwa kusudi la Mungu, umeleta kionjo cha kipekee katika muziki wa Injili mwaka 2024.

Japhet ameweka wazi kuwa wimbo huo mpya uliotoka mwanzoni mwa wiki hii, tayari mashabiki wameupokea vizuri katika majukwaa yote ya muziki ikiwa ni pamoja na chaneli yake ya YouTube.

" Nimekuwa kimya muda mrefu sababu kuna mambo nilikuwa nayaweka sawa, sasa nimeanza kazi rasmi na kutakuwa na mfululizo wa nyimbo mpya yaani 'back to back'. Pia Zabron Singers kama timu tunajiandaa kufanya albamu mpya mwaka huu na taarifa rasmi itatoka maandalizi yakikamilika," amesema Japhet.

## Otile afafanua kilichomtokea



MWANAMUZIKI wa kizazi kipya kutoka nchini Kenya, Otile Brown, amesema kuna watu wamelipwa na wabaya wake ili kumdhalilisha anapotumbuiza katika majukwa mbalimbali.

Akizungumza na mashabiki wake kupitia TikTok, Otile Brown, amesema kwamba tukio la wiki iliyopita ambapo alionekana akizomewa na mashabiki, lilipangwa na watu hao ili kukamilisha njama zao mbaya.

"Shoo ilikuwa vizuri tu, ni hapo mwanzo tu na ambapo waliichukua na kuikata ikawa vile, kwa sababu nilikuwa nimeambiwa nina dakika saba za kutumbuiza. Walikuwa na 'intro' yangu na wakati wanaicheza sikuisikia hivyo ikanichochea kurudi nyuma kwa sababu sikuwa najisikia," Otile alifafanua.



# ROMA MKATOLIKI AWAPONDA MARAPA

MWANAMUZIKI maarufu wa Hip Hop nchini, Roma Mkatoliki amesema wasanii wengi wa muziki huo hawana uwezo wa kuandika nyimbo zao katika utaratibu uliokamilika.

Mkatoliki amemtetea swahiba wake Stamina kwamba licha ya watu kumtuhumu kwamba uandishi wake ni wa kitoto, lakini yeye anamkubali kutokana na kuwa na kila kitu kinachotakiwa wakati akiandika nyimbo zake.

"Kaka angu Stamina baadhi ya raia wanamkaanga sana wakimsema Uandishi wake (Word Play) kuwa ni wa kitoto. Binafsi napenda anachokifanya kwa sababu tuna rapa wengi tu wana uandishi wao sio tu wa kitoto, bali hauna uhalisia wowote" amesema Mkatoliki.





# Miwani anayovaa Nyoshi usipime

MKALI wa muziki wa dansi nchini, Nyoshi El Sadaat, amesema kila anachokitumia katika mwili wake kina gharama kubwa kiasi ambacho mtu anayetaka kushindana naye hataweza kumfikia.

Amesema kila kitu kwake kinatumia pesa nyingi na kutolea mfano miwani anayovaa kwa kila siku inamgharimu kiasi cha Sh. milioni.

"Nimeingia Tanzania 1992 mpaka leo natumia mkorogo ni pesa ngapi? Usifikiri natumia mkorogo wa 50,000, mimi natumia kuanzia laki tatu kwa chupa moja pekee, ukipiga hesabu hapo kwa mwaka mmoja naweza kujenga nyumba zaidi ya tatu kwa pesa ninazozitumia kujitunza," amesema Nyoshi.

# BADO NAKUPENDA SIONI

**Na Adam Fungamwango**

"NIAMBIE, bado nakupenda, sioni Side." Unaweza ukadhani kuwa haya maneno ameambiwa mtu mmoja na mpenzi wake. Hapana. Hizi ni ngoma tano zilizorekodiwa mwezi Machi.

Haya ni majina ya ngoma 'zilizotrendi' mwezi uliopita zikitolewa na wasanii mbalimbali.

Hebu twende tuangalie ngoma moja baada ya nyingine, siku ilivyotolewa na msanii gani aliyeitoa.

### Niambie-Macvoice

Ngoma hii ilitolewa Machi 12 na msanii Macvoice ambapo awali aliitoa kwenye mfumo wa audio, lakini baadaye akaitoa kwa mtindo wa video na imeanza kushika chati, ikiteka mashabiki wengi wa bongo fleva.

### Bado-Jux

Hii ndiyo ngoma ya mwisho kutoka kati ya hizi tano, yenyewe ilifyatuliwa Machi 21 na msanii mkongwe Jux.

Ni moja ya pini za mwezi Machi ambazo kwa sasa zinatrendi sana kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari, kama redio na televisheni.

### Nakupenda-Beka Junior

Beka Junior hakukaa kimya mwezi Machi, yeye tarehe nane tu alifyatua ngoma yake kali, akaita 'Nakupenda.'

Nayo si haba, imekuwa ikitikisa kwenye mitandao ya kijamii na kwenye maeneo yote ambapo ngoma za bongo fleva zinapatikana.

### Sioni-Nay wa Mitego

Ngoma hii ya Nay wa Mitego, ndiyo ya kwanza kutoka mwezi Machi, ilikiwa imeipuliwa studio tarehe tatu na kuwekwa hadharani.

Ni ngoma ambayo pia amemshirikisha msanii Kusah, na tayari imeshaanza kuwa gumzo kwa mashabiki wa bongo fleva nchini.

### Side Nigga-Harmonize

Machi 14, mmoja wa wasanii wakubwa nchini, Harmonize akatoa ngoma yake aliyoiita,' Side Nigga.'

Imeshaanza kuchukua kijiji, kutoka kwa mashabiki wa muziki huo na kuendelea kumuweka msani huyo juu mawinguni.





FILAMU

# Mume Bwege, Mke Mjinga

**Na Adam Fungamwango**

SINA utaalam sana wa mambo haya, lakini kwenye vitabu vya dini kuna andiko moja huwa nalisikia sana, mwanamke mpumbavu ataivunja nyumba kwa mikono yake mwenyewe.

Ni kweli kabisa, ndani ya jamii yetu wapo wanawake ambao walishaondokana na kuzurura, wameshasitirika, lakini wakaamua kuvunja ndoa zao na sasa wanahangaika.

Filamu ya 'Mume Bwege,' inaakisi kile ambacho ninakisema hapa. Ni somo au fundisho kwa wanawake wote waliokuwa kwenye ndoa. Siku zote mbuzi hawezi kuona thamani ya mkia wake mpaka pale utakapokatwa.

Imechezwa na Dorah Martin, Rayuu Chande, Nyama Ega, Devi Chilumba, Chato Pera na wengineo.

Chilumba alikwenda kijijini na kumuona binti mmoja aitwaye Dora. Miezi kadhaa tu baadaye Dora akavamia mji kwa pupa. Mji nao ukampokea. Akawa hasikii la muadhini wala mnadi swala. Akajigeuza na kujifanya mtoto wa mjini, anayejua ya usiku na ya mchana.

Kikubwa zaidi na hata aliyemleta mjini akamfanya bwege. Akamuweka kiganjani mumewe, sijui kwa mapenzi, au limbwata dada, mume akaanza kupika, kuchota maji, kufua nguo mpaka za mkewe.

Wakati huo yeye ni kiguu na njia kwa mashoga zake, kwenye ngoma, vigodoro, ili mradi tu nyumbani hakukaliki.

Vyote anamfanyia mumewe anakwenda kumhadithia shoga yake Rayuu ambaye hajaolewa.

Kumbe vyote anavyomgadithia, binti yule roho inamuuma. Yeye anaitaka ndoa lakini haipati. Anamhitaji mwanaume ambaye atamtunza lakini wapi. Akaazimia kumkomesha rafiki yake.

Wakati anarejea nyumbani akiwa na mizigo mingi, huku mkewe akiwa amekakataa katakata kuja kumpokea stendi, Chilumba njiani anakutana na Rayuu.

Shemeji yake haraka akampokea mizigo na kumsindikiza kwa umbali mrefu, mpaka walipokaribia kufika akampa mizigo yake akitakaa kufika nyumbani kwa kumhofia mkewe.

Kitu kile kilimliwaza mno, Chilunda, akagundua kubwa kumbe bado wapo wanawake dunia hii wanaothamini na kuenzi wanaume.

Taratibu, akaanza kumuwaza Rayuu badala ya mkewe. Penzi likamuingia na Rayuu akalipokea.

Dora akapata bwana ambaye alimshawishi amuache mumewe, alipofanya hivyo haraka, Chilumba akamtwaa Rayuu.

Waliposhindwana huko, Dora akarejea nyumbani na kumkuta amemrithi. Hakuamini, ikawa ni kilio na kusaga meno.




# Swift anaishi dunia nyingine

MUZIKI umemlipa msanii wa Pop, Taylor Swift, baada ya kuingia katika orodha ya watu matajiri duniani.

Kulingana na jarida la Forbes, mwanamuziki huyo anakisiwa kuwa na utajiri wa dola za Marekani bilioni 1.1 na kushika nafasi ya 2,545 kwa watu wenye ukwasi wa fedha.

Hata hivyo imeelezwa, Swift amepata utajiri huo kutokana na kazi ya muziki na hasa matamasha yake yaliyomwingizia kiasi cha dola milioni 190 baada ya ushuru kufikia sasa.



## Schwarzenegger afanyiwa upasuaji

GAVANA wa zamani wa California na mwigizaji maarufu wa filamu za Terminator, Arnold Schwarzenegger, amefanyiwa upasuaji wa kuwekewa kifaa maalumu cha kuongoza utendaji kazi wa moyo.

Schwarzenegger ambaye ana miaka 76, amewaambia mashabiki zake kutokuwa na hofu kutokana na upasuaji huo kwenda vizuri na kila siku afya yake inazidi kuimarika.

"Upasuaji umekwenda vizuri, kwa sasa moyo wangu upo kama mashine, kifaa cha pacemaker kimenisaidia kuwa imara zaidi," amesema Schwarzenegger.

## Voughan amekwenda zake

ALIYEKUWA rais wa waongozaji wa filamu nchini Nigeria, Frank Igho Okpokoro Vaughan, amefariki dunia.

Kulingana na taarifa ya Mwenyekiti wa sasa wa chama hicho, Victor Okhai, amesema Vaughan ambaye pia ni mwandaaji maarufu wa filamu alifariki juzi.

Vaughan, alizaliwa 1960s, kuna kipindi alikuwa mchungaji katika kanisa la Dominion City, katika mji wa saba, ulioko jimbo la Delta State.

Pia alikuwa mwongozaji wa tamthilia katika televisheni na kazi hiyo aliifanya katika ubora wa kimataifa.





## Shakira aonja tamu na chungu

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Colombia, Shakira, ameingia kwenye vichwa vya habari baada ya kueleza kwamba filamu yake inayoitwa Barbie, licha ya kumpatia mafanikio, imewaathiri watoto wake wa kiume.

Katika mahojiano na jarida la Allure, mwanamuziki huyo ambaye anaishi Marekani, amesema filamu hiyo iliyoongozwa na Greta Gerwig, imempatia dola bilioni 1.4 kutokana na mauzo ulimwenguni kote na pia kuingia katika uteuzi wa tuzo nane za Oscar.

Alionyesha kutoridhishwa kwake kuhusu athari za filamu hiyo kutokana na hisia hasi za wanawe wawili wa kiume ambao walionekana kuchukizwa na nafasi aliyocheza kama mhusika mkuu.

## Terry utaishi vipi bila ndoa?

MKALI wa muziki wa Afrobeats kutoka Nigeria, Terry G, amefichua kuwa hatarajii kuoa kwa sababu mke anaweza kuathiri muziki wake.

Akizungumza hivi karibuni, mwimbaji huyo wa kibao cha 'Akpako', alisema kuwa ndoa na muziki havichanganyiki na mtu anayeamua kuingia katika maisha hayo lazima awe mwaminifu.

"Sijaoa lakini sifikirii kabisa kufunga ndoa, haipo kwenye mipango yangu, nina miaka 37 na sijawahi kuoa, nadhani sio kwa ajili ya watu kama sisi wanamuziki," alisema.





# Bosi wa TEHAMA ahadharisha madhara matumizi yasiyo sahihi mifumo kidijitali

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

TUME ya TEHAMA Tanzania (ICTC), imesema kutokuwapo kwa matumizi sahihi ya mifumo ya kidijitali, kunaweza kusababisha kutwezwa kwa utamaduni wa taifa na utu wa Watanzania.

Hatua hiyo ni kutokana na kuruhusu taarifa za siri za serikali, kampuni na za mtu binafsi kupatikana kwa utaratibu usio sahihi; kisha kutumiwa na watu wasiokuwa na dhamana ya kutumia taarifa husika.

Pia imesema dhana ya mabadiliko ya tabia za binadamu na matumizi ya teknolojia za kidijitali, haziwezi kufanikiwa endapo mifumo ya kidijitali, itakuwa kikwazo kwa ukuaji uchumi na ukuaji wa biashara za kampuni na shughuli za mtu mmoja mmoja.

Mkurugenzi Mkuu wa ICTC, Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema hayo juzi jijini hapa katika jukwaa la tatu la usalama wa mitandao linalowashirikisha wataalam, watunga sera na viongozi wa viwanda.

Alisema malengo ya mageuzi ya kidijitali, hayawezi kufikiwa endapo suala la usalama wa mitandao linalowezesha matumizi salama ya huduma za kidijitali, halitapewa uzito unaoendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA).

Jukwaa hilo lililowashirikisha wadau 350 kutoka kampuni mbalimbali, washirika wa maendeleo na mashirika yasiyo ya kiserikali, lilichagizwa na mada kutoka kwa Mshauri wa Ulinzi wa Taarifa kutoka Ujerumani, Dk. Tino Naumman na Mshauri wa Serikali wa Masuala ya Mitandao wa Estonia, Margus Magi.

Tanzania inashika nafasi ya pili barani Afrika, nyuma ya Mauritius, kwa kuwa kinara wa masuala ya usalama wa mtaandao,

Kaulimbiu ya mwaka huu inasema 'Kutengeneza Dunia ya Mtandao Iliyo Jumuishi na Shirikishi'.

"Sote tunafahamu kwa suala la mageuzi ya kidijitali ni endelevu na mtambuka, hivyo sote kwa pamoja hatuna budi kuendelea kuchukua hatua za makusudi za kutunga na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na mikakati inayolinda usalama wadau wote walio katika ikolojia ya kidijitali (Digital Ecosystem) kuanzia serikali mpaka mtu mmoja mmoja.

"Umadhubuti wa mfumo wa kisheria, utajengwa na maendeleo ya ubunifu wa mbinu mbalimbali za kitaalamu za kuhakikisha kuwa Tanzania iko katika ulimwengu wa kidijitali ulio salama.

"Usalama wa mtandao una mahusiano makubwa na uwekezaji; ambapo kwa Tanzania tumeanza kupata mafanikio makubwa katika uwekezaji kutokana na juhudi zinazoendelea katika usalama wa mtandao," alisema.

Kuhusu matumizi ya akili mnemba, Dk. Mwasaga alisema kuwa teknolojia hiyo haiwezi kufanya kazi bila kupata taarifa.

Katika jukwaa hilo, Mwenyekiti wa Bodi ya ICTC, Prof. Leonard Mselle, alisema ufundi wa kidigiti kwa kwa sasa ndio ufundi mkubwa kuliko ufundi wowote ule duniani, ambao umesababisha kugunduliwa kwa teknolojia ya akili mnemba (AI).

" Tanzania kama sehemu ya dunia, hatuwezi kuacha kujijengea uwezo katika kuelekea uchumi wa kidigiti, kwa kuwa dunia nzima inaelekea humo ikiwa ni pamoja na kutoa huduma mbalimbali, zikiwemo za kijamii, kiserikali na binafsi," alisema.

Mkufunzi wa TEHEMA kutoka Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Sakina Seleman, alisema jukwaa hilo la siku mbili lina umuhimu mkubwa, hasa kwa wanawake kutokana na changamoto kubwa iliyopo kwa sasa ya masuala ya ukatili wa kimtandao kwa wanawake.

"Mimi kama mtaalam wa masuala ya mtandao tumepata fursa nzuri kupitia Jukwaa hili ya kujadili kwa kina jinsi ya kufanya mtandao iendelee kuwa salama katika nchi yetu pamoja na watumiaji," alisema.

Jumatano wiki hii, wakati Rais Samia Suluhu Hassan anazindua Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, alitoa miezi sita pamoja na maelekezo matano kwa Wizara husika na taasisi za umma, kuhakikisha mifumo ya TEHAMA iwe imesomana.

Aliagiza tume hiyo kuhakikisha taasisi zote za umma na binafsi zinasajiliwa na kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kabla ya mwezi Disemba mwaka huu.




Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki (kulia), akizungumza baada ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Burian (katikati), kuwasili wilayani humo jana, kwa ajili ya ziara ya kukagua miradi itakayopitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru. Wengine ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina (kushoto) na (wapili kushoto) ni Mkuu wa wilaya hiyo, Zainabu Abdallah. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Hatima ya kesi ya Pauline Gekul Aprili 15

**Na Godfrey Mushi,** BABATI

HUKUMU ya kesi ya rufani iliyofunguliwa na Hashim Ally katika Mahakama Kuu, Kanda ya Manyara, dhidi ya Mbunge wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul, imepangwa kutolewa Aprili 15, mwaka huu.

Gekul anakabiliwa na kesi ya unyanyasaji dhidi ya aliyekuwa mfanyakazi wake, Hashim Ally.

Kwa mujibu wa hati ya wito ya kuitwa shaurini Wakili wa Hashim Ally, Peter Madeleka, hukumu hiyo itasoma saa 8:00 mchana Aprili 15, mwaka huu na Jaji Devota Kamuzola anayesikiliza kesi hiyo.

Mwezi uliopita, mahakama hiyo ilisikiliza mapingamizi matatu ya upande wa utetezi katika kesi hiyo.

Mapingamizi hayo yaliwasilishwa katika mahakama hiyo na Wakili Ephraim Kisanga anayemwakilisha Gelul katika shauri hilo la rufani ya jinai, namba 577 ya mwaka 2024.

Pingamizi la kwanza lilikuwa la mahakama hiyo kukosa mamlaka ya kisheria ya kusikiliza rufani iliyotolewa na mrufani Hashim Ally.

Kwa mujibu wa Wakili Kisanga, pingamizi lao la pili ni kwa mtoa rufani, alishindwa kutafuta njia nyingine mbadala ya kisheria tofauti na rufani.

Pingamizi la tatu ni kuhusiana na notisi (ilani) iliyotumika kufungulia kesi ya msingi, ambayo ni rufani namba 577, ilikuwa haikidhi vigezo vya kisheria kuitwa notisi.

Mrufani katika kesi hiyo Hashimu Ally, anawakilishwa na Wakili Peter Madeleka, anayesaidiwa na Wakili Thadey Lister na John Masanja.

Aidha katika shauri la msingi, Gekul alikuwa akikabiliwa na shtaka moja la shambulio na kusababisha madhara kwa mwili, chini ya kifungu cha 241 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Marekebisho ya Mwaka 2022.

Alikuwa anadaiwa kuwa yeye na watu wengine ambao hawako katika malalamiko hayo, Novemba 11, 2023 mjini Babati, mkoani Manyara, walimwita Hashim na kumweka kizuizini.

Pia wanadaiwa kumtishia kwa silaha ya moto, kumvua nguo na kumshambulia kwa kumlazimisha kukalia chupa ya soda ili iingie katika njia yake ya haja kubwa.

# Wahabesh jela miezi 18 kuingia bila kibali

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Manyara, imewahukumu wahamiaji haramu 20 raia wa Ethiopia, kutumikia kifungo cha mwaka mmoja na nusu kila mmoja au kulipa faini Sh. milioni moja kila mtu kutokana na kosa la kuingia nchini bila kufuata taratibu za kisheria.

Akisoma hukumu hiyo jana, Hakimu Mkazi Martine Masaho, alisema washtakiwa hao walikamatwa Machi 23, mwaka huu, katika kizuizi cha polisi Minjingu, wilayani Babati mkoani Manyara wakisafirishwa kwenda Afrika ya Kusini.

Aidha mshtakiwa wa pili hadi wa 20, walipewa nafasi ya kujitetea na wote walikiri kwa nyakati tofauti kuingia nchini bila kufuata taratibu za kisheria.

Baada ya kukiri waliiomba mahakama kuwapunguzia adhabu kutokana na kosa walilolifanya.

Wakati wao wanahukumiwa mshtakiwa namba moja, dereva aliyekuwa akiwasafirisha, Edward Erihard, kesi yake itatajwa Aprili 30, mwaka huu, kutokana na kukana mashtaka na ataendelea kuwa nje kwa dhamana.

Naye Wakili wa Serikali, Rose Kayumbu, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaokiuka sheria.

Hakimu Masaho baada ya kusikiliza pande zote mbili aliwatia hatiani kwenda jela kutumikia kifungo cha mwaka mmoja na nusu kila mtu au kulipa faini ya shilingi milioni moja kila mtu.

Waethiopia hao na dereva aliyekuwa akiwasafirisha, walisomewa mashtaka Machi 28, mwaka huu.

Awali, Hakimu alianza mapema kusikiliza kesi hiyo lakini iliahirishwa kwa muda baada ya mkalimani aliyekuwa akitafsiri lugha ya kiethiopia, mawasiliano yake kukatika na baadaye yaliporejea, kesi iliendelea.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Unakumbuka redioni, vipindi mashairi, ombi lako, tumbuizo asilia, chei shangazi?

**Na Adam Fungamwango**

TULIPOWAZUNGUMZIA Mabingwa wa Salaam enzi hizo kwenye redio ya Taifa, ikiitwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD), baadhi ya wasomaji walipiga simu na wengine kutuma meseji wakitaka siku vizungumwe pia vipindi pendwa na maarufu enzi hizo.

Wasomaji wengi wameeleza kukumbuka mbali sana, wakisema kuna baadhi ya vipindi vinawakumbusha mbali sana, hasa walipokuwa wanasikia nyimbo zake.

Wakasema baadhi ya nyimbo huwakumbusha bakora shuleni, zingine walivyokuwa wakitumwa dukani, au kwenda shambani na wazazi wao, na wapo waliosema baadhi ya vipindi vinawakumbusha kipindi ambacho wanarejea shule.

Kuna waliosema baadhi ya vipindi huanza muda ambao wamerejea shuleni wakati mwingine maharage hayajaiva, hivyo wanaambia waokote kuni, au vifuu kwa wale wa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kwa ajili ya kuendelea kuchochea mpaka yaive kabla chakula hakijapikwa.

Wachangiaji wengine wakasema kuna vipindi ambacho nyimbo zake zikisikika hadi leo wanaanza kusikia njaa, kwa sababu hupigwa muda wa mchana ambao wanarejea shuleni, na vipo vipindi vinavyowachukiza kwa sababu ndiyo muda ambao huamka kwenda shuleni.

Ni kweli kabisa kipindi hicho nchini redio ni moja tu, hivyo vipindi vyote utake usitake usikiliza tu, labda uzime redio.




Aina ya redio maarufu zaidi ya zamani kuliko zote, iitwayo 277, ambayo Wabongo wengi walikuwa wakisikiliza vipindi mbalimbali kupitia redio hii.

Na kila kipindi kilikuwa na kipande chake cha wimbo kutoka kwenye kibao cha wimbo wa bendi fulani. Na kwa kweli kipande chochote kilichochukuliwa lazima kilikuwa maarufu.

Ukiondoka vile vya alfajiri ambavyo ni vya dini, na baadaye Kumekucha.

Hiki kipindi kilisababisha wimbo wa 'Kumekucha', uliopigwa na Safari Trippers, ukiimbwa na Marijani Rajab uchukiwe, kwa sababu kilianza saa 11:30 hadi saa 12:00, muda ambao wanafunzi wanatakiwa waamke na kujiandaa kwenda shule.




Aina nyingine ya redio iliyotumika kusikiliza vipindi mbalimbali na redio RTD zamani, ila hii ilikuwa na muundo tofauti, ikiwa na mfuko wake pamoja na kamba, ambapo inaweza kubebwa kama begi, au kuitundika juu ya mti.

Kitendo kuusikia wimbo huo muda huo ina maana kipindi hicho kinaanza au kinaisha na mwanafunzi anatakiwa kuamka.

Kulikuwa pia na vipindi kama Asubuhi Njema, baadaye kikabadlishwa kikaitwa Jambo, baada ya hapo inakuja 'Tuimbe Sote', na kuna wakati kunakuwa na vipindi vya shule, huku siku maalum, kulikuwa na 'Misakato' siku ya Ijumaa, ambapo miziki mipya sita, iliyorekodiwa na moja ya bendi zilizokuwapo nchini kipindi hicho pamoja na uchambuzi wake.

Hapo ndipo safari ikifika saa tano, kunakuwa na kipindi cha Wakati wa Kazi, wakihojiwa wafanyakazi zaidi wa taasisi za kibiashara, huduma za umma na viwandani, baada ya kuongea na watangazaji hupewa fursa ya kuchagua wimbo.

Cha kushangaza asilimia 70 ya waliokuwa wakiomba nyimbo, wimbo wao mkubwa ulikuwa ni 'Salamu Baba na Mama.' Kila wiki haukusosa kupigwa kutokana na kuombwa mara nyingi.

Inapotimu saa sita, ndiyo kinasikika kipindi cha Mchana Mwema, ambacho hufuatiwa na Taarifa ya Habari saa Saba Mchana, muda huo sehemu kubwa ya watumishi hasa viwandani, walirudi nyumbani kwa mlo na kurejea tena makazini saa nane mchana.

Unaweza kujiuliza walipataje muda huo kwa miji kama Dar es Salaam? Idadi ya wakazi, haikuwa kama ilivyo sasa, wengi walirudi na mabasi ya mashirika yao, na hata tabia ya kutembea kwa mguu ilizoeleka mno, na Dar haikuwa pana kama ilivyo sasa, vitongoji kama Mbezi, Pugu, Tegeta, na Buza kote kulikuwa shamba. Hapo hatujajadili, aina ya mlo tunaoukuta nyumbani, maharage yasioiva na ubwabwa uliojaa mchaga, au ubwbwa wa changa za unga, usisindikizwa na vinywaji togwa, na maji yasiyochemshwa yanayochotwa mtungini. Ila maajabu yake, maji mabombani yalikuwa hayakauki.

Mchana huo kunakuwa na kipindi chz salamu, kinachoitwa Mchana Mwema, na baada ya hapo sasa vinakuja vipindi fulani vilivyochukiwa sana na watu.

Na hata hii leo vimebaki kuwa simulizi wa watu wazima na sasa pindi wanapovikumbuka.

Vipindi hivyo ni Malenga wa Mashairi, Tumbizo Asilia, Misitu ni Uhai na vingine amabvyo havikuorodheshwa hapa.

Si kwamba vilikuwa vipindi vibaya, la hasha. Ila vilikuwa vinaanza mida ya saa saba mpaka saa nane mchana au tisa hivi. Ni kipindi ambacho waliokuwa wanafunzi, hasa wa shule za msingi na sekondari ndiyo walikuwa wanatoka shuleni.

Na kwa sababu wanakuwa na njaa, wanapopita njiani kuelekea nyumbani unakuwa ndiyo muda wa vipindi hivyo. Kama nilivyosema awali, wakati mwingine hata ukifika nyumbani mchakato wa kupata msosi wa mchana unakuwa mrefu sana.

Kwa maana hiyo hadi leo hii wapo waliotuma meseji wakisema, wanaposikia vipande vya nyimbo hizo wanaanza kuhisi njaa, wakikumbuka jinsi ilivyokuwa enzi hizo.

Tukija wikiendi tunakutana na vipindi kama Zilipendwa. Kumbuka kuwa ni zamani, miaka ya 1970, 1980, hadi mwishoni mwa 1990, lakini kulikuwa na kipindi hicho. Ina maana ilipigwa miziki ya zamani ambayo ni nyuma zaidi ya miaka hiyo.

Kukawa na vipindi kama Chei Chei Shangazi, ambacho kilikuwa ni cha watoto wanafunzi wakihojiwa kutoka mashuleni kwao, baada ya hapo kunakuwa na kipindi cha Ugua Pole.

Kipindi hiki walihojiwa wagonjwa wananakuwa wamelazwa katika hospitali mbalimbali nchini.

Wagonjwa pia walikuwa wakipewa nafasi ya kuchagua wimbo. Cha ajabu wimbo wao mkubwa waliouchagua ulikuwa ni 'Siku ya Kufa' wa Orchestra Makassy.

HABARI KIMATAIFA

# Serikali Niger yavunja mabaraza yote ya miji

**NIAMEY,** NIGER

KIONGOZI wa kijeshi wa Niger, Jenerali Abdourahamane Tiani, ameamuru kuvunjwa kwa mabaraza yote ya miji nchini humo na amemteua ofisa wa jeshi kusimamia mji mkuu wa Niamey.

Kulingana na vyombo vya habari vya serikali, Jenerali Tiani, ambaye alimuondoa madarakani rais wa taifa hilo katika mapinduzi yaliyofanyika Julai 2023, alitia saini amri ya kuvunjwa kwa mabaraza ya manispaa na majimbo.

Mabaraza hayo yalichaguliwa kwa mara ya mwisho mwaka 2020.

Pia Redio ya serikali ilitangaza amri ya pili ya kiongozi huyo ambayo ilitaja majina ya wanajeshi, polisi na maofisa wa umma watakaosimamia serikali za mitaa.

Miongoni mwa viongozi walioondolewa ni meya wa mji mkuu wa Niger, Oumarou Dogari, ambaye nafasi yake imechukuliwa na kanali wa jeshi.

**DW**

# Marekani yaonyesha wasiwasi na China

**BEIJING,** CHINA

WAZIRI wa Fedha wa Marekani, Janet Yellen, ameonya kwamba ruzuku zinazotolewa na serikali ya China kwa viwanda vyake zinaweza kuvuruga uchumi duniani.

Katika ziara yake nchini China, Yellen alielezea wasiwasi wake kuhusu uzalishaji wa kupita kiasi unaofanywa na kampuni za China hasa kwenye uundaji wa vyombo na vifaa vya kielektroniki vinavyoelemea soko la dunia.

Akizungumza na Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Marekani mjini Guangzhou, Yellen alisema angejadiliana na China kuhusu changamoto zinazokabili biashara za Marekani nchini humo.

**Dw**

# Israel yakubali kuifungua Gaza

**TEL AVIV,** ISRAEL

BAADA ya kubanwa na mataifa rafiki, hatimaye Israel imekubali kufungua njia mbili zitakazotumika kuingizwa kwa misaada ya kibinadamu Ukanda wa Gaza.

Njia itakayofunguliwa ni ya Erez iliyoko kaskazini mwa Gaza, ambayo itakuwa mara ya kwanza kutumika tangu kuanza kwa vita na Bandari ya Ashdod pia itaanza kazi ya kupakua na kusafirisha misaada.

Aidha, misaada mingine itaruhusiwa kutoka Jordan kuingia kituo cha mpakani cha Kerem Shalom.

Kufunguliwa kwa njia hizo kunatokana na mazungumzo yaliyofanywa jana na Rais wa Marekani, Joe Biden na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyau.

Mazungumzo hayo yalifanyika kwa mara ya kwanza tangu kuawa kwa wafanyakazi saba wa shirika la kimataifa la World Centre Kitchen.

Rais Biden alionya kuwa Israel lazima ichukue hatua kuzuia madhara ya raia na mateso ya kibinadamu ikiwa inataka uungwaji mkono na nchi yake.

Ilielezwa kwamba kufunguliwa upya kwa njia hizo kunatokana na maombi ya Rais Biden wakati wa ,mazungumzo hayo waliyofanya kwa njia ya simu.

Kiongozi huyo wa Marekani aliipa serikali ya Israel kauli ya mwisho ambayo ni kuchukua hatua madhubuti kuzuia madhara kwa raia na kuhakikisha usalama wa wafanyakazi wa misaada au sera ya nchi hiyo itabadilika kuhusu vita hiyo ya Gaza.

Hatua hiyo ni mabadiliko makubwa katika sera ya Marekani na kwa mara ya kwanza imejaribu kutumia misaada yake ili kushawishi mwenendo wa vita.

Wakati huo huo, mfumo wa GPS ulizimwa katika maeneo mengi ya Israel jana ili kuepuka mashambulizi ya makombora na ndege zisizo na rubani kutoka Iran.

Nchi ya Iran imeapa kulipa kisasi baada ya mashambulio katika jengo la ubalozi wake mdogo wa nchini Syria.

Tukio hilo lililotokea Jumatatu na kusababisha vifo vya watu watatu, iliaminika Israel inahusika kuwa nyuma ya shambulizi.

Vikosi vya Ulinzi vya Israel (IDF) pia vilitangaza kusitisha likizo zote kwa wanajeshi wanaofanya kazi katika vitengo vya vita.


Hatua hiyo inakuja siku moja baada ya askari wa akiba kuitwa jeshini ili kuimarisha vitengo vya ulinzi wa anga.

Mamlaka za Israel zinaonekana kuamini kuwa jibu la Iran liko karibu na linaweza kutekelezwa Ijumaa, ambayo ni Siku maalumu ya Quds au Siku ya Jerusalem.

Siku hiyo mara nyingi imekuwa ikitumika kuandaa mikutano ya wafuasi wa Palestina wanaoipinga Israel katika nchi ya Iran.

Raia wa Israeli waliripoti kuwa hawakuweza kutumia huduma za programu hiyo katika maeneo ya miji mikubwa kama Tel Aviv na Jerusalem.

**BBC**



Gari la zima moto likiwa limeharibiwa vibaya na mashambulizi ya droni za Russia kwenye mji wa Kharkiv ulioko mashariki mwa Ukraine jana. **PICHA. REUTERS**

# Sierra Lione yatangaza 'Kush' kuwa janga la taifa

**FREETOWN,** SIERRA LIONE

RAIS wa Sierra Leone, Julius Maada Bio, ametangaza kuwa matumizi ya dawa za kulevya ni janga la kitaifa na kutaka kukabiliana na aina ya dawa hizo zinazopendwa na vijana.

Dawa za kulevya zinazopendwa kutumiwa na vijana ni Kush, ambayo ni mchanganyiko wa dawa yenye athari sawa na bangi na tramadol ambayo imezidi kuenea nchini humo kwa miaka mingi.

"Nchi yetu kwa sasa inakabiliwa na tishio lililopo kutokana na athari mbaya za matumizi na uraibu wa dawa za kulevya, haswa kush," alisema Rais Bio

Kiongozi huyo alisema katika hotuba kwa taifa aliyoitoa Alhamisi, kuwa Kush ni dawa iliyoleta athari mbaya kwa jamii.

Alisema serikali yake inajitahidi kusambaratisha mitandao ya makundi ya walanguzi wa dawa za kulevya nchini humo.

Dawa hiyo ambayo pia inajulikana kama K2 inapatikana kwa urahisi na vijana wasio na ajira wanaokabiliwa na changamoto ya umaskini.

Wataalamu wa afya walionya kuwa ulaji wa kush unaweza kusababisha uharibifu wa kudumu wa ubongo na kuongezeka kwa vitendo vya kujiua.

Mwezi Februari, serikali ya Sierra Leone ilianzisha kituo cha kurekebisha tabia kwa waathiriwa wa matumizi ya dawa za kulevya na kuunda kikosi kazi cha kupambana na hali hiyo kilichowajumuisha mawaziri.

Nchi jirani za Guinea na Liberia pia wanapigania kuzuia ongezeko la matumizi ya kush.

Rais mpya wa Liberia, Joseph Boakai, hivi karibuni alitangaza matumizi ya dawa za kulevya kuwa ni janga la kiafya na kutangaza kamati ya kukabiliana na tishio hilo.

**BBC**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-7

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

Ni mwanamke ambaye kila mwanaume alitamani kuwa naye. Sura yake ya mviringo, rangi yake maji ya kunde, mashavu ambayo yalikuwa na vishimo ambavyo vilijidhihirisha wazi pale anapocheka.

Uzuri wake hapo unaongezeka kwa mwanya, uliojiegemeza kwenye mpangilio mzuri na meno meupe kama theluji.

Pua yake ilikuwa mchongoko, na kushoto kwake kiliota kidoti cheusi ambacho kiliendelea kuupamba urembo wa msichana huyo.

Macho yake peupe ya duara malegevu, yaliwafanya wanaume kuona kama yanawaona hadi ndani ya mioyo yao.

Alikuwa na umbile namba nane, hipsi zilionekana vizuri, na nyuma ya sura yake alikaa vizuri na kuwa kivutio si kwa wanaume tu bali hata kwa wanawake wenzake.

Nao walikuwa wakimuona walikubali kuwa pamoja na kwamba nao ni warembo, lakini mwenzao amependelewa.

Mwili wake pia ulikubali nguo yoyote aliyoivaa. Ilikuwa ni saa 1:00 usiku, baada ya kutumia karibuni dakika 20 nzima kuvaa, alienda kujiangalia tena kwenye kioo na kuridhika kuwa sasa anaweza kutoka.

Alikuwa anakwenda kukagua na kuchukua mahesabu ya pesa kwenye vitega uchumi vyake.

Alipotoka nyumbani mlangoni, akakata upande wa kulia ambako kulikuwa na njia ya kwenda barabarani ambako angechukua bodaboda.

Ghafla akahisi kama kuna kitu au mtu nyuma yake. Kabla hajageuka kutazama kuna nini alipigwa na kitu kizito kichwani.

Alichoona hapo mwanzo ni nyota nyota nyingi nyekundu, baadaye giza totoro. Kilichofuata akahisi kutumbukia kwenye shimo kubwa ambalo halikuwa na mwisho.

******************************

"Ndugu Waandishi wa Habari, habari zenu. Leo tuna taarifa ya kifo cha msichana mmoja aliyefahamika kwa jina la Mariamu Salumu. Kwa mujibu ya taarifa tuliyoletewa ni kwamba alifariki alfajiri ya jana baada ya kuanguka maeneo ya Tabata Bima akiwa anafanya mazoezi.

Taarifa zinasema mwanadada huyu ana kawaida ya kufanya mazoezi na inasemekana wakati anakimbia, alianguka, kwa bahati mbaya akaangukia kitu kizito kisogoni ambacho kimesababisha kifo chake.

Timu yetu yamaaskari ilikwenda kuchukua mwili wa marehemu na kuukuta ukiwa na nguo za mazoezi, fulana na suruali ya michezo, pamoja na raba. Wanasema waliikuta maiti yake kwenye mtaro, pembeni ya barabara."




**Mkanganyiko huo ndiyo uliowafanya ndugu kulalamika kuwa Jeshi la Polisi lianzishe uchunguzi kwa kina kwa sababu kuna upotoshaji mkubwa aliopewa Kamanda.**

Ilikuwa ni sauti ya Kamanda wa Kanda Maalum ikitangaza au kuelekezea kifo cha msichana Mariamu.

Tetesi ya kifo chake ilienea kama moto wa nyika maeneo yote ya Tabata zote, Segerea, Bima, Kimanga na vitongoji wake.

Hakuna aliyeamini kama msichana mzuri na mrembo kama yule anaweza kukatika kama mgomba unavyokatwa na kisu na mwenyewe anapoamua.

Ni kwa sababu jana yake walimuona. Akiwa mzima wa afya. Kutokana na hilo, ndipo kila mmoja sasa anayetoa taarifa akawa anasema amepata ajali ya gari. Wengine na bodaboda. Ili mradi tu kila mtu alitaka kuwa na kwanza kuitangaza habari hiyo kwa jinsi anavyojua yeye.

Pamoja na yote hayo, taarifa hiyo ya msiba ilitikisa. Ilimuuma kila mmoja aliyekuwa anamfahamu popote pale alipo, kuanzia wakubwa mpaka watoto. Wanaume mpaka wanawake wenzake.

"Kweli kifo hakijali uzuri wako, kifo kinamchukua yoyote yule, hakuna cha umaarufu, wala ubondia, kifo ni siri kubwa sana." Mama mmoja alisema kwa namna ya kuomboleza akiwa ameshika kichwa, baada ya kusikia taarifa hiyo.

Kamanda akiwa anaonekana kwenye televisheni zote nchini alipigilia msumari wa mwisho kwa wale ambao walikuwa hawaamini, wakiona labda wanaoeneza taarifa hiyo ni waongo, au kuna mtu mwingine anayefanana na yeye.

"Kwa sasa napenda kuwaambia kuwa kwa mujibu ya taarifa tulizoletewa na hizo, lakini sisi kama Jashi la Polisi tutaendelea kufanya uchunguzi.

Msishtuke Waandishi wa Habari na hata wananchi, hii ni kawaida wa Jeshi la Polisi, hata kama tukimkuta mtu ndani amejinyonga na ikaonekana kuwa ameandika mwenyewe barua kuwa amefanya hivyo kwa sababu binafsi na hakuna anayehusika, bado huwa tunafanya uchunguzi kwa sababu kwenye dunia hii chochote huwa kinafanyika. Mtu anaweza kulazimishwa kuandika, halafu akauawa. Mkisema muache tu, mnakosesha haki kupatikana na muuaji anaendelea kuwa uraiani," alisema Kamanda, akawaangalia Waandishi wa Habari kwa zamu, halafu akaendelea.

"Sisemi kama kwa kifo hiki ndivyo ilivyotokea, hapana, ila huu ni utaratibu, na uchunguzi utaanza baada ya ripoti kamili ya madaktari hapo ndipo tutakapoanza. Wao watatuambia kitaalam wanaonaje, maana binti inaonekana alikuwa anafanya mazoezi, akaanguka, kwa hiyo ni mshtuko wa moyo, alisukumwa na gari, au alikuwa na shida yoyote ya kiafya," alisema Kamanda na hapo akawa amemaliza.

****************************

Baadhi ya ndugu wa Mariamu walionekana kupingana na taarifa ya kamanda. Wakadai aliletewa taarifa isiyo sahihi. Na wakaazimia kususia maiti mpaka hapo watapopata ripoti kamili kutoka kwa daktari.

Zipo taarifa walizozinyaka kuwa ndugu yao hakuonekana tangu usiku wa kumkia siku ambayo inasemekana alikuwa anafanya mazoezi alfajiri akaanguka.

Kuna taarifa kuwa kuna mtu alikuja nyumbani kwake saa sita ya usiku na kumgongea, lakini hakukuwa na majibu. Je alilala wapi? Na huku akikolala ndiyo asubuhi akaamkia jogging?

Mkanganyiko huo ndiyo uliowafanya ndugu kulalamika kuwa Jeshi la Polisi lianzishe uchunguzi kwa kina kwa sababu kuna upotoshaji mkubwa aliopewa Kamanda.

Mwingine aliyekuwa na wasiwasi ni Kamal. Mpenzi wa Mariamu. Mara ya mwisho inasemekana aliongea na mpenzi wake ambaye alimwambia anakata atoke nyumbani ili akakague na kufunga biashara zake.

Baada ya nusu baadaye simu ilikuwa haipatikani. Haikupatikana kwa muda mrefu ambapo si kawaida yake.

Akaamua kwenda nyumbani wake. Kamal na Mariamu pamoja na kwamba ni wapenzi, lakini kila mmoja bado anaishi kivyake, bado hawakuwa wameanza kukaa pamoja.

Kamal akaamua kumfuata Mariamu na bodaboda hadi nyumbani kwake. Ilikuwa ni saa sita usiku. Akagonga lakini wapi. Simu nayo haipatikani. Kitu cha kwanza alichofanya ni kuamua kufungua mlango na kuingia ndani. Kamal alikuwa na funguo zote za nyumba anayoishi mpenzi wake.

Alipoingia ndani aliona dalili zote za Mariamu kuondoka hapo. Pamoja na kwamba anamuamini sana, lakini akaanza kuwa na wasiwasi kuwa anazoziona sasa ni dalili za usaliti.

Hata hivyo, katika pekuapukua aliikuta simu ya Mariamu ndani. Ni kama alikuwa ameisahau hivi kwa sababu ilikuwa mezani. Akili yake ikamtuma kuwa alikuwa ameisahau na si vinginevyo.

Hata hivyo kilichomshtua ni kwa nini hajarudi kuichukua? Vyovyote iwavyo, isingewezekana mtu aliyesahau simu akakaa zaidi ya masaa manne hajarejea kuifuata. Hii ikazidi kumtia wasiwasi kuwa huenda yupo kwenye matatizo zaidi, na si kama anavyodhani kuwa amekwenda kwa bwana.

**Itaendelea Jumamosi**

HABARI MICHEZO

# SERIKALI, TBF KUFUNGUA 'UKURASA MPYA' KIKAPU

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

SERIKALI kwa kushirikiana na Shirikisho la Kikapu Tanzania (TBF), limesema linajipanga kuwekeza zaidi katika mchezo huo ili kukuza viwango vya wachezaji wake kwa lengo la kushindana kitaifa na kimataifa, imeelezwa.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinyijuma 'Mwana FA' wakati wa uzinduzi wa jezi wa Timu ya Taifa ya Kikapu uliofanyika jijini, Dodoma juzi.

Mwana FA alisema kikapu ni mchezo muhimu sana hivyo serikali iko katika mstari wa mbele kuhakikisha unasonga mbele.

„Serikali itashirikiana na TBF kwa ajili ya kuhakikisha mpira wa kikapu unasonga mbele,"alisema Mwana FA.

Naibu Waziri huyo amewataka viongozi wenye dhamana ya kuongoza mchezo huo kuweka wazi changamoto zinazowakabili ili kwa pamoja wakutane kuzijadili na kuzifanyia kazi.

Alisema kuna michezo aina sita ambayo iko katika mikakati ya kuhakikisha inafanya vizuri kama ilivyo upande wa mpira wa miguu.

Aliongeza mpira wa kikapu unapaswa kuchezwa katika viwango vya ushindani kuanzia ukanda wa Afrika mashariki na Afrika yote.

Alielekeza ili kufikia malengo, kunatakiwa kuwa na viwanja vya kutosha vya mchezo huo ambavyo vitatumika watakapoandaa mashindano mbalimbali.

Kuhusu ujenzi wa viwanja vya mchezo vya kisasa, Mwana FA alisema baadhi ya viwanja vya soka vitakavyojengwa pia vitakuwa na viwanja vya kikapu.

Naye Rais wa TBF, Michael Kadebe, alisema jezi zilizozinduliwa ni moja kati ya maandalizi ya kuingia makubaliano na Alex Kajumulo na kuongeza hatua hiyo inadhihirisha mchezo huo unaendelea kukua.

Kadebe alisema maandalizi ya mashindano ya Kombe la Taifa (Taifa CUP) yanaendelea vizuri na kutaja michuano hiyo kwa mwaka huu itafanyikia jijini, Dodoma.

Kiongozi huyo aliishukuru serikali kwa ushirikiano inaowapa wadau wa michezo na kupelekea michezo mbalimbali kuimarika kwa kiasi kikubwa.




Wachezaji wa Pamba FC ya jijini Mwanza wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya Fountain Gate Academy. Timu hiyo iliyoko katika mbio za kupanda daraja imebakiza mechi tatu kumaliza msimu. **PICHA: MTANDAO**

# Ligi ya Wanawake Aprili 15

**Na Saada Akida**

MZUNGUKO wa pili wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania utaanza rasmi kuanzia Aprili 15, mwaka huu ambapo mabingwa watetezi, JKT Queens watakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo kuwakaribisha Bunda Queens kutoka mkoani Mara.

Vinara wa ligi hiyo, Simba Queens yenyewe itakuwa ugenini kuwavaa Ceasiaa Queens kwenye Uwanja wa Samora ulioko Iringa huku Geita Gold Queens wakiwakaribisha Alliance Girls katika dimba la Shule ya Sekondari Nyakumbu.

Mchezo mwingine wa ligi hiyo utakuwa kati ya Amani Queens dhidi ya Fountain Gate FC Princess utakaochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi na Yanga Princess watakuwa nyumbani dhidi ya Baobab Queens kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar-es-Salaam.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema timu zote zinazoshiriki ligi hiyo zinaendelea na maandalizi ya mzunguko wa pili baada ya mapumziko mafupi ya kupisha ratiba ya timu ya Taifa kumalizika.

„Ligi ya Wanawake inarejea Aprili 15, mwaka huu, tunaimani timu zinafahamu na ratiba wanazo, wanaendelea kujipanga kuelekea mechi za duru la pili," alisema Ndimbo.

Katika msimamo wa ligi hiyo Simba Queens wanaongoza wakiwa na pointi 25, nafasi ya pili inashikiliwa na JKT Queens yenye pointi 21 na Yanga Princess wanafuatia wakiwa na pointi 18, nafasi ya nne ikikamatwa na Ceasiaa Queens wenye alama 16.

Bingwa wa ligi hiyo atawakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), ili kusaka timu itakayowania tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake baadaye mwaka huu.

# Julio : Macho yangu Ligi Kuu Tanzania Bara

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya Tabora United, Kocha Mkuu wa Singida Fountaine Gate, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema jukumu lake kubwa alilopewa ni kuinusuru kushuka daraja na si kutwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA.

Kwa matokeo hayo, Tabora United imetinga hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la FA ikiungana na Namungo FC ya Lindi.

Singida Fountain Gate ikiwa nyumbani kwenye Uwanja a CCM Kirumba jijini, Mwanza juzi ilipokea kichapo hicho na kuondolewa katika michuano hiyo ambayo bingwa atapata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo, Julio alisema pamoja na michuano ya Kombe la FA ni muhimu, lakini hakuiweka katika mipango yake kwa sababu kazi kubwa iliyompeleka Singida Fountain Gate ni kuibakisha kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na si vinginevyo.

Julio alisema anawaandaa wachezaji wake kuhakikisha hawapotezi pointi katika mechi zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara ili kujiondoa kwenye janga la kushuka daraja.

„Tumefungwa katika mechi ya Kombe la FA ambayo kwangu mimi si muhimu, ingawa nilikuwa nahitaji kupenya, ila silitilii maanani kwa sababu siyo kazi iliyonileta, kitu kilichonileta mimi katika klabu hii ni kuinusuru Singida isishuke na tumeanza vizuri kwa ushindi wa bao 1-0 tukaifunga Namungo," alisema Julio.

Beki huyo wa zamani wa Simba alisema jambo lililomgharimu na kusababisha kupoteza mechi hiyo ni kucheza pungufu kutokana na mchezaji wake mmoja kutolewa kwa kadi nyekundu.

Naye Kocha Msaidizi wa Tabora United, Mrundi, Masoud Djuma, alisema licha ya kuwa na siku chache tangu waichukue timu lakini wanashukuru Mungu wamepata ushindi na kutinga hatua ya robo fainali.

„Kilichotusaidia sana ni wachezaji wetu wametumia nafasi ambazo wamezipata, na tulitaka wachezee zaidi eneo la mpinzani kuliko kwetu," alisema Djuma, kocha wa zamani wa Simba na Dodoma Jiji FC.

Julio alitua Singida Fountain Gate baada ya mabosi wa timu hiyo kumtimua Thabo Senong, raia wa Afrika Kusini pamoja na benchi lake la ufundi lililokuwepo.

Mabao ya Tabora United iliyoko hoi katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye mechi ya juzi yaliwekwa wavuni na Najim Mussa, Patrick Lembo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

### SILVA AITAMANI BARCA

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Joao Felix, amesema mchezaji mwenzake wa kimataifa, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 29 anataka kuhamia Barcelona, huku kiungo huyo wa kati wa Manchester City akihusishwa na klabu hiyo ya Katalunya mara kadhaa. (***Gerard Romero***)

### AMORIM ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imeanza mazungumzo na Kocha wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, mwenye umri wa miaka 39 ili kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp pale Anfield. (***Foot Mercato***)

### AMORIM ALITAJWA BARCA

BARCELONA pia ilikuwa inamtaka Kocha, Ruben Amorim, lakini imesitisha mpango huo kwa sababu wanafikiri huenda akaelekea Liverpool. (***Sport***)

### KONSA KUTUA VILLA

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua mlinzi wa Aston Villa, Ezri Konsa, mwenye umri wa miaka 26. (***Footbal Transfers***)

### ATALANTA YAIKANA LIVERPOOL

KLABU ya Atalanta imesema haijapokea mawasiliano yoyote ya moja kwa moja kutoka kwa Liverpool, kuhusu kiungo wao Mholanzi Teun Koopmeiners, akiripotiwa kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (***90 min***)

### VALVERDE KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL inataka kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Federico Valverde, mwenye umri wa miaka 25 ambaye kwa sasa anaichezea Real Madrid. (***Team Talk***)

### ZIRKZEE AIKATAA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Bologna na Uholanzi, Joshua Zirkzee, mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akinyatiwa na Manchester United na Liverpool, lakini amemwambia wakala wake angependelea kuhamia AC Milan. (***Mirror***)

### ARSENAL, UNITED VITANI

ARSENAL inajiandaa kupambana na Manchester United katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa Barcelona mwenye umri wa miaka 19, Mikayil Faye. (***Calciomercato, via TeamTalk***)

### MANTATO SAFI UNITED

KLABU ya Manchester United imempa mkataba mpya winga, Bendito Mantato, mwenye umri wa miaka 16 huku timu nyingine mbalimbali maarufu pia zimetajwa kumwinda kinda huyo. (***Fabrizio Romano***)

### EVERTON MAMBO MAGUMU

KLABU ya Everton huenda ikapunguziwa pointi kwa mara ya tatu baada ya ripoti ya akaunti zake za hivi punde kutolewa. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG AFUNGUKA SIRI INAYOWAMALIZA

## Kocha huyo aeleza wachezaji wa United hawajui kumaliza mechi...

**LONDON, England**

ERIK ten Hag alisema wachezaji wa Manchester United wanapaswa kujua namna ya kuimaliza mechi baada ya kuanguka kwenye kipigo kingine cha kushangaza cha mabao 4-3 ugenini dhidi ya Chelsea hapo juzi usiku.

United walidhani walikuwa wametengenezea ushindi wa kukumbukwa wao wenyewe, kwa kuruhusu mabao mawili ya mapema tu na kusawazisha kabla ya Alejandro Garnacho kufunga la tatua ambalo lilionekana goli la ushindi.

Kikosi cha Ten Hag kilidumisha uongozi wao hadi dakika za lala salama, lakini wakaporomoka katika dakika za mwisho, huku Cole Palmer akikamilisha hat-trick yake kwa mabao mawili ya dakika za mwisho, la kwanza kwa penalti, na tena muda mfupi baadaye kufunga la nne pale katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye dimba la Stamford Bridge.

Bao la ushindi la Palmer katika dakika 101 liliweka rekodi kama bao la hivi punde la kushinda mchezo katika historia ya Ligi Kuu, kwa mujibu wa takwimu na taarifa za ESPN.

Ni mechi ya pili mfululizo kwa United kupigwa na butwaa katika dakika za mwisho, huku Brentford wakifunga bao la dakika ya 99 katika mechi yao ya mwishoni mwa wiki na kupata sare.

**"Ulikuwa mchezo mzuri kwa wasio na upande wowote," aisema Ten Hag akiiambia BBC Sport baada ya mechi". Mchezo mzuri wa soka wenye ubora mwingi.**

„Manchester United walitawala mchezo, lakini tulifanya makosa ya kibinafsi ambayo yalitugharimu mchezo. Tunapaswa kujifunza kutokana na hilo. Unapokuwa mchezaji wa United unapaswa kujua jinsi ya kukabiliana na hali hii."

Matokeo hayo yanamaanisha United hawakutumia nafasi ya Tottenham Hotspur na Aston Villa walipoteza pointi wiki hii, na hivyo kuzima matumaini ya United kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

„Kwa muda wa siku tano tulipoteza pointi tano. Hilo halikubaliki. Tunapaswa kuwa na kiwango cha juu ikiwa tunataka kuwania kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya," aliongeza Ten Hag.

„Sijui kama nafasi nne za juu zimeondoka. Ni lazima niangalie tena nafasi hiyo. Pointi zitakuwa ghali zaidi. Inasikitisha sana tunafanya hivi na kufanya maamuzi yasiyo sahihi. Tuliachana na mchezo ambao tulipaswa kushinda."

United walipiga mashuti 28 na kufikisha jumla ya mikwaju 107 katika mechi zao nne zilizopita katika michuano yote. Hata hivyo, Ten Hag tena alisema hana wasiwasi na shinikizo kwenye lango la United.

Kazi ya United haitakuwa rahisi katika mchezo wao unaofuata, kwani watacheza na viongozi wa Ligi Kuu England, Liverpool kwenye Uwanja wa Old Trafford hapo kesho.

## HABARI MICHEZO




# PARTEY : SINA MPANGO WAKUONDOKA ARSENAL

**LONDON,** England

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Thomas Partey amesisitiza "ninafuraha" licha ya tetesi zinazomhusisha za kutaka kuihama klabu hiyo.

Partey alianza dhidi ya Luton Town Jumatano usiku akiwa amekosa sehemu kubwa ya msimu wa 2023/24 hadi sasa kutokana na majeraha.

Mkataba wake unamalizika 2025 na amekuwa akihusishwa na uhamisho kutoka hapo kwenye dimba la Emirates, huku Hispania, Italia na Saudi Arabia mara nyingi zikitajwa kuwa na uwezekano wa yeye kutua.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 amefutilia mbali uvumi yuko tayari kuhama majira ya joto na amedokeza huenda akatafuta mkataba mpya Arsenal.


Akizungumza baada ya kuichezea Arsenal kwa mara ya kwanza tangu Agosti, Partey alisema: „Kichwa changu huwa hapa. Hapa ndipo ninapochagua kucheza, nina furaha sana kila ninapokuwa uwanjani.

„Najua uvumi mwingi umekuwa ukiendelea, lakini kwangu, nina furaha sana kuwa hapa na kuendelea kuichezea klabu hii. Pamoja na mkataba wangu, bado nina hadi mwisho wa msimu, nadhani. Lazima nifanye niwezavyo na kujaribu kucheza kwa kiwango cha juu na nadhani jambo la muhimu zaidi ni kupatikana kila wakati."

Partey ameichezea Arsenal mechi tisa pekee msimu huu, na ana matumaini ya kuingia kwenye kikosi hicho watakapomenyana na Brighton & Hove Albion kwenye Ligi Kuu England leo Jumamosi.

# Ramsdale, Newcastle United kitaeleweka

**LONDON,** England




KLABU ya Newcastle United imerejea tena kutaka kumnunua mlinda mlango wa Arsenal, Aaron Ramsdale, ripoti mpya imedai.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amepoteza nafasi yake kwenye Uwanja wa Emirates kwa David Raya, ambaye yuko kwa mkopo kutoka Brentford, baada ya kukaa kwa misimu miwili kama kipa chaguo la kwanza wa klabu hiyo.

West Ham United pia imekuwa ikimfuatilia Ramsdale, ambaye anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake baada ya Euro 2024 msimu huu wa joto huku kukiwa na nia ya klabu nyingine kutoka Ulaya.

Tovuti ya 90min imeeleza Ramsdale, ambaye alijiunga na Arsenal mwaka 2021 kwa dili la pauni million 30, angependelea kubakia katika Ligi Kuu England, na Mail Sport iliripoti Newcastle inaweza kumpa njia nyingine kutoka London Kaskazini wakati wanataka kuimarisha kikosi chao.

Kocha, Eddie Howe, tayari amemsajili Ramsdale mara moja katika maisha yake ya soka, wakati akiwa Bournermouth, na inadaiwa mipango ya uhamisho ya Newcastle ni pamoja na kuleta mbadala wa makipa wawili, Martin Dubravka na Nick Pope.

Dubravka (35), kwa sasa anamiliki glavu huko Tyneside, huku Pope (32), akiendelea kupata nafuu kutokana na bega lake lililoteguka wakati wa mechi iliyofanyika Desemba mwaka jana dhidi ya Manchester United, lakini mkataba wa Mslovakia huyo una zaidi ya mwaka mmoja tu kukamilika.

Ramsdale ameichezea Arsenal mechi sita pekee za Ligi Kuu England msimu huu baada ya kuwasili kwa Raya.

# United, Chelsea zamwinda Mendy

**LONDON, England**

CHELSEA na Manchester United zote zimetajwa kuwania saini ya beki wa kushoto wa Real Madrid, Ferland Mendy kwa mujibu wa ripoti ya nchini Hispania.

Mendy alijiunga na Madrid akitokea Lyon mwaka wa 2019, lakini sasa nafasi yake pale Santiago Bernabeu iko hatarini huku Madrid ikitafuta kumsajili, Alphonso Davies, kutoka Bayern Munich.

Huku Mendy akiingia katika mwaka wa mwisho wa mkataba yake msimu huu wa joto, maswali yameulizwa juu ya hatima yake huko Madrid, na kwa mujibu wa Mundo Deportivo, Chelsea na United wote wanatazamia kumnunua Mfaransa huyo majira ya joto.

Uwezekano wa Davies kuwasili Madrid utamfanya Mendy kuachwa kwenye nafasi ya ziada na na pia wanaweza kuwa na matumaini ya kurejesha fedha ambazo zingehitajika kumsajili Davies.

Kuna mgawanyiko nyuma ya pazia, Kocha, Carlo Ancelotti anajulikana kuwa shabiki mkubwa wa Mendy.

Bosi huyo mara nyingi amemtaja Mendy kama „beki wa pembeni bora zaidi duniani" kama inavyosemekana kushinikiza mkataba mpya kukabidhiwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

Iwapo Mendy atapatikana kwa ajili ya uhamisho, ripoti zinazitaja Chelsea na United kujaribu kumsajili, huku timu zote za Ligi Kuu England zikifahamika zinamwinda beki mpya wa kushoto.

Chelsea, ambao walianza kampeni wakiwa na ziada ya mabeki wa kushoto, wanatarajia kuwauza Lewis Hall na Ian Maatsen msimu huu wa joto na pia wanatarajiwa kupokea ofa kwa Marc Cucurella.

Kuondoka kwa wote watatu kutamuacha Ben Chilwell pekee kama beki wa kushoto mkuu kikosini.

Kwa upande wa United, Erik ten Hag tayari ana mabeki wawili waandamizi wa kushoto, Luke Shaw na Tyrell Malacia, lakini wawili hao wanakabiliwa na majeraha msimu huu.



# Azam FC, Mtibwa zatambiana

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema amefanya maandalizi mazuri kuelekea mechi ya hatua ya 16 Bora ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Mtibwa itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Dabo aliliambia gazeti hili vijana wake wapo tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi na hatimaye kusonga mbele katika michuano hiyo.

Kocha huyo alisema licha ya kupata matokeo mazuri mara mbili dhidi ya Mtibwa Sugar, anaamini mchezo wa kesho hautakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wao hawatakubali kupoteza tena kwa mara ya tatu.

"Huu ni mchezo wa mtoano na kila mmoja anahitaji kutafuta ushindi ili kusonga mbele, wachezaji wangu wapo tayari kukabiliana na Mtibwa Sugar," alisema Dabo.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo licha ya kikosi chake kuwa katika kipindi kigumu cha kukosa ushindi kwenye michezo ya Ligi Kuu.

Katwila alisema wanatambua ubora wa Azam FC na sababu hiyo wamejipanga vizuri kuhakikisha wanafanikiwa kupata matokeo na kuwashangaza wenyeji wao.

"Hakuna mechi rahisi katika hatua hii ambayo kila timu iliyofika iko vizuri na anaimani na vijana wake watafanya vyema kwa kuyahamisha mafunzo ya mazoezi kwenye uwanja wa mechi," alisema kocha huyo.



# SINGIDA FOUNTAIN GATE YAIPIGA MIKWARA YANGA

**Na Adam Fungamwangu**

ILI kuhakikisha inajiondoa katika hatari ya kushuka daraja, Singida Fountain Gate imesema haitakubali kupoteza mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga itakayochezwa Aprili 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hussein Massanza, amesema kuifunga Yanga ni moja kati ya ajenda zao 10 ambazo wanatarajiwa kuzitelekeza kabla ya kumaliza mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Massanza alisema baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo, ajenda hayo inayofuata namba mbili ni kushinda mechi hiyo dhidi ya Yanga ambayo itawaimarisha katika kutimiza malengo ya kubakia Ligi Kuu.

„Tulianzisha agenda 10, hizo ni mechi ambazo tumebakiwa nazo, tumeweka malengo ya kushinda mechi zote hizo, au kama ikipungua sana tuvune hata pointi moja, lakini si kupoteza hata mchezo mmoja, tulianza kwa Namungo, sasa tunakwenda kwa Yanga na wengine wote watakaokuja wajiandae," alisema Massanza.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Jamhuri Kihwelo ‚Julio', amesema hawaihofii Yanga na watakwenda kupambana kwa tahadhari kwa sababu wanahitaji kuondoka na matokeo chanya.

„Tumejiandaa na tumejipanga vizuri, Yanga ni timu inayofungika kama tutakwenda kwa mipango na maelekezo. Siyo kama tukicheza na Yanga yaani tayari wameshatufunga, wanafungika kabisa hakuna matatizo yoyote, tutakabiliana nao kwa ajili ya kusaka ushindi," alisema Julio.

Baada nyingine za Singida Fountain Gate zilizobakia ambazo zimewekwa katika mpango wao wa ajenda 10 ni dhidi ya Ihefu FC itakayochezwa Aprili 18, mwaka huu na baadaye itawakabili Mashujaa FC utakaopigwa Aprili 18 halafu itapambana na Coastal Union Mei 2, mwaka huu.

Mei 7, mwaka huu Singida Fountain Gate itakutana na Dodoma Jiji wakati mechi dhidi ya JKT Tanzania, KMC na Geita Gold bado hazijapangiwa tarehe lakini Mei 29, mwaka huu itakuwa na mchezo dhidi ya Kagera Sugar.

Yanga ndio vinara na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (wa pili kushoto), akikabidhi vifaa vya michezo kwa timu zitakazoshiriki mashindano ya Bonnah Segerea Cup 2024 yanayoandaliwa na Mbunge wa Jimbo la Segerea, Bonnah Kamoli (kushoto). Timu 64 zilizoko katika jimbo hilo lililoko jijini, Dar es Salaam zitashiriki michuano hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mayele : Ninaweza kujiunga Simba SC*

„Al Ahly wale wa zamani si wa

INATOKA UK. 24

sasa, unajua wao hawajabadilisha wachezaji, wachezaji ni wale wale wa zamani, wao ni binadamu, wanachoka, wanacheza mashindano mengi, ...kuna wachezaji wanapaswa kuamua matokeo, kuna Chama (Clatous)," aliongeza mshambuliaji huyo.

Kutokana na safu yake ya ushambuliaji kutofanya vyema, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, alilazimika kutumia siku tano baada ya mechi ya mkondo wa kwanza ya robo fainali kuwanoa mastraika kwa ajili ya mchezo wa jana usiku.

Benchikha aliandaa dozi maalumu kwa lengo la kutumia vyema kila nafasi itakayopatikana na hatimaye Simba kufikia malengo yake.

Katika kuboresha safu ya washambuliaji ya Simba, wakati wa dirisha dogo iliwasajili Fred Michael na Pa Omar Jobe, ambao bado hawajaonyesha makali yanayotakiwa na kikosi hicho.

Simba pia inaamini bado inaweza kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo linashikiliwa na watani zao, Yanga huku pia Azam FC ikiwa kwenye vita ya kumaliza msimu wa 2023/2024 katika nafasi mbili za juu.

# Aziz Ki, Kouassi...

INATOKA UK. 24

KMC, aliyetoa pasi tano mpaka sasa.


Mabeki watano wanaofuatia waliotoa asisti ni Paschal Msindo, Lusajo Mwaikenda (Azam), Shomari Kapombe , Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr' (Simba) na Nickson Kibabage wa Yanga.

Baada ya kumalizika kwa mechi za hatua ya 16 Bora ya mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake atapata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, michezo ya Ligi Kuu Bara itarejea tena wiki ijayo.


# Michezo

Jumamosi Aprili 6, 2024

Nipashe

Ten Hag afunguka siri inayowamaliza UKURASA 21



Wachezaji wa Chelsea wakishangilia bao la ushindi katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Manchester United iliyochezwa kwenye Uwanja wa Stamford Bridge juzi usiku. Chelsea ilishinda mabao 4-3. **PICHA: MTANDAO**

# Mayele : Ninaweza kujiunga Simba SC

**Na Saada Akida**

## ●●● Mkongomani huyo awaambia Msimbazi lolote linawezekana lakini…

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Pyramids FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Misri, Fiston Mayele, amesema lolote linawezekana kuhusiana na uamuzi wa kujiunga na Simba katika msimu ujao wa 2024/2025.

Mayele alijiunga na Pyramids mwaka jana baada ya kuichezea Yanga kwa mafanikio ambapo msimu uliopita aliisaidia kucheza fainali za mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mshambuliaji huyo amekuwa akihusishwa kutakiwa na Simba kwa ajili ya msimu ujao ili kuimarisha safu ya ushambuliaji ambayo kwa sasa ni tatizo linalowasumbua zaidi Wekundu wa Msimbazi.

Akizungumza baada ya kutembelea kambi ya Simba nchini Misri ambayo jana usiku iliwakabili wenyeji, Al Ahly katika mechi ya marudiano ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Mayele alisema mpira ni kazi yake na muda utakapofika kila kitu kitawekwa wazi.

**„Kwa kweli tumuombe Mungu, tumalize msimu, na Inshaa Allah chochote kinawezekana,“ alisema kwa kifupi mshambuliaji huyo wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Mkongomani huyo alisema amefanikiwa kuitazama Simba katika mashindano ya kimataifa na kuona ina tatizo katika safu ya ushambuliaji ambayo ingekuwa vyema, ilikuwa na uwezo wa kuamua matokeo kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa Dar es Salaam.

Alisema katika mashindano makubwa safu ya ushambuliaji ndio huamua matokeo kwa sababu michezo hiyo ni ya kutumia kila nafasi zinazopatikana.

„Mimi kama mchezaji niliangalia mechi ya kwanza Tanzania, wenzangu walipambana, Simba walitengeneza nafasi, lakini hawakuzitumia vizuri. Siongei hayo kwa sababu mimi ni mshambuliaji bali kwa kuwa nimeangalia michezo wa kimataifa," Mayele alisema.

Nyota huyo alisema Al Ahly ya msimu huu si ile yenye makali kama ilivyokuwa zamani kwa sababu imetumia wachezaji wale wale kwa muda mrefu.

INAENDELEA UK. 23



Mayele

# Aziz Ki, Yao Kouassi na ufalme wa Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akitwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Machi, nyota huyo ameendelea kuwa kinara wa mabao katika Ligi Kuu Tanzania, usaidizi wa upatikanaji magoli, huku beki wa timu hiyo, Yao Kouassi akiongoza kwa kutoa pasi za mwisho kwa upande wa mabeki.

Kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Ligi, Aziz Ki, raia wa Burkina Faso ambaye ana ‚hat-trick‘ moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara amefunga mabao 13 sawa na Feisal Salum ‚Fei Toto‘ wa Azam FC.

Hata hivyo, Aziz Ki, anaongoza kwa kuchangia jumla ya mabao 20 kwenye Ligi Kuu, ikiwa ni idadi ya juu zaidi mpaka sasa, kwa sababu pamoja na kufunga mabao ana asisti saba, huku mwenzake Fei Toto akiwa na asisti tano.

Takwimu zinasema Fei Toto amechangia jumla ya mabao 18 ya kufunga na kutoa pasi za mwisho, huku Kipre Junior wa Azam akichangia mabao 14, ambapo wachezaji watano wanafuatia wakiwa wamefanya hivyo mara 11.

Wachezaji ambao wamefunga mabao ukijumlisha na ‚asisti‘ zikifika 11 ni Clatous Chama wa Simba, Marouf Tchakei (Singida Black Stars), Pacome Zouzoua, Maxi Nzengeli wote wa Yanga na Waziri Junior wa KMC.

Kwa maana hiyo Nzengeli mwenye mabao tisa ana ‚asisti‘ mbili, Tchakei ana magoli nane ana ‚asisti‘ tatu, Pacome mwenye mabao saba, ametoa pasi nne za mabao, na Chama aliyefunga mabao sita, yeye ana ‚asisti‘ tano.

Kwa upande wa Kouassi, anawaongoza mabeki wote wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kutoa ‚asisti‘, anazo saba mpaka sasa na anafuatiwa na Rahim Shomari wa

INAENDELEA UK. 23



9 770856 541002 >